KAZI NI IMANI KATIKA MATENDO

Asante. Ni vema kuwa mahali hapa, usiku huu, tena. Sikujua walipataje kujua ya kwamba nitawaombea wagonjwa. Kila mtu amekuja kuombewa. Unajua, ninaamini kama ukifuata uongozi wa Roho, ni sawa. Huo ni bora kabisa, huo ndio Ujumbe usioshindwa kamwe.

2 Sasa, leo nilikuwa nimeketi chumbani, baada . . . mhudumu fulani ninayempenda sana kwa moyo wangu (watatu), watatu wa marafiki wangu wazuri sana, waliniambia walikuwa wanakuja kula chakula cha mchana pamoja nami. Nami nikawaza, "Vema, hilo lilikuwa ni sawa tu," unajua.

3 Kwa hiyo ni—nilikula tu kiasi kidogo cha kiamshakinywa kwa kuwa nilikuwa na hakika watakilipia, mnaona, na mimi . . . nina mlo kamili wa mchana. Kwa hiyo saa 6:00 ikafika, na saa 7:00 ikafika, na saa 8:00 ikafika, bado hakuna mtu aliyekuja. Kwa hiyo kulikuwa na . . . polisi walikuwa wakifukuza mhalifu, huko maeneo ya uani, na kwa hiyo nikashuka kwenda nikaone kisa hicho. Sikuweza kumwona Ndugu Jack kabisa. Kwa hiyo, nikaja kutambua, huyo mtu wa hoteli alikuwa amempa namba nyingine; naye alikuwa akipiga kengele kwenye mlango mwingine, wakati wote, mahali ambako si—sikuwa. Nitampa nafasi anilipie, mara nyingine tena, haidhuru, wakati mwingine. Yeye na Ndugu Tracy, hakika nilifurahi kuwaona wao na Ndugu Brown usiku wa leo. Hilo linaonekana tu kana kwamba inatupasa kurudi Arizona tena.

4 Ninaweza kukumbuka tulipokuwa tukivuka jangwa hivi majuzi. Nilimwambia mke wangu, kule nyuma, nilisema, "Hapa ndipo Ndugu Jack alipoketi nyuma ya Chevrolet hii ndogo." Yeye na Ndugu Brown walibishana sana juu ya u—uumbaji wa asili, iwapo ulifanyika katika siku sita ama iwapo ulifanyika katika miaka milioni sita. Hilo lilikuwa la kuchekesha kweli.

5 Walibishana sana, hata wakatoka nje na kuokota konzi ya mawe, na mmoja akaenda nyuma ya nguzo moja, na mwingine nyuma ya nyingine, na kurushiana mawe kwa nguvu walivyoweza. Hawakuweza kulisuluhisha namna hiyo, kasema, "Ninaweza kukushinda mbio." Haoo wanakimbia barabarani mbio; Ndugu Jack, maskini jamaa mfupi, akatimua mbio akijisokota alivyoweza kujisokota; na Ndugu Young akiwa na hiyo miguu mirefu, mwajua. Sijapata kucheka sana namna hiyo maishani mwangu!

6 Halafu, Ndugu Jack alikuwa amerudi kwenye gari na kuvua viatu vyake. Ndugu Sherritt alikuwa ametupatia gunia kubwa la machungwa, naye akafagia nusu yake kabla hatujafika Shreveport.

7 Mnajua, hizo ni siku nzuri mno, hata hivyo. Naam, bwana, ni siku nzuri mno. Ninajua linasikika la kiutani, la kuchekesha, bali ni kweli. Lakini sisi . . . kuna jambo fulani kuhusu hayo, jinsi unavyozidi kukua na unaanza kuwazia mawazoni mwako. Unawazia juu ya siku hizo ambazo ulitamani ungeweza kuziishi tena, hiyo ni kweli, siku za ujana wetu. Na tunavyozidi kuzeeka, hayo yote yanakuwa ni taswira. Ninafuraha sana zilikuwa ni safi na takatifu, na za ushirika wa ndugu, katika upendo. Tukijua ya kwamba tunaenda kwenye nchi ambako hatutazeeka, ambako . . . ile Nchi kuu, kule ng'ambo, ambako kamwe hatutakuwa wazee wala hatutakufa hata.

8 Mmoja wa ndugu zetu wa thamani, mpenzi sana kwetu sote, yeye alivuka tu majuzi akaingia kwenye Nchi ile. Na kila ninapokuja kwenye jukwaa hili, na—nadhani nitawazia juu ya Ndugu Lyle. Niliangalia kote jana usiku na nikamwona maskini Judy ameketi pale, na moyo wangu ulikuwa tu ukinienda mbio, nilikuwa nikiwazia jinsi alivyokuwa akijisikia. Nami najua wakati baba yangu alipokufa jinsi . . . Lakini inatubidi tu kupitia katika vipindi hivyo vya mateso kujua jinsi mtu huyo mwingine anavyojisikia.

9 Ninaamini ninamwangalia mhudumu mmoja rafiki yangu wa siku nyingi ambaye anaketi hapa. Siwezi kabisa kukumbuka jina lake. Hiyo ni kweli, ulikuwa ukiwaombea wagonjwa hapa, wakati wote, miaka mingi iliyopita? [Mtu fulani anasema, "Gerholtzer."—Mh.] Gerholtzer, hilo—hilo jina la Kijerumani, si—sikuweza hata kidogo kulitamka vizuri. Ndugu Tracy alikuwa amekutana naye kule nje. Nami nilimjua kama miaka kumi hivi, ndipo nikasema, "Hujazeeka kiasi cha miezi sita katika hiyo miaka kumi." Tunaishi katika ulimwengu ambao hauna budi kukoma siku moja.

10 Sasa, usiku wa leo, nilikuwa . . . Niliwachelewesha sana jana usiku, nitajaribu nisifanye hivyo usiku huu. Hebu nimalize hadithi yangu; nilikuwa nikiwazia, usiku huu, kuhubiri juu ya so—somo la *Unyakuo*, kwa kanisa. Jinsi vile hali, kama ninavyoliona katika Maandiko, kwamba itabidi Kanisa liwe katika hali gani kwa ajili ya Kunyakuliwa, na yale yatakayotukia kabla tu Kunyakuliwa hakujatukia, na jinsi kutakavyotukia. Na sisi sote tunaamini katika Kunyakuliwa, sivyo? Tunaamini katika jambo hilo. Na basi, kwa ghafla, kitu Fulani kikasema tu, "Ombea wagonjwa, usiku wa leo." Nami nilikuwa tu nikila chakula cha mchana pamoja na maskini ndugu mmoja wa Kimeksiko pale, nikashuka kwenda na kumchukua hapo barabarani. Nadhani yuko hapa usiku wa leo, yeye na mkewe.

11 Na baadaye mtu fulani akaja, na akanipa ushuhuda. Kasema, "Kama . . . Kwenye maeneo ama kanisani," akasema, "kuna mtu pale, ambaye, ninaamini ilikuwa kama mwaka mmoja uliopita, ambapo alikuwa amekuja kwenye mstari wa utambuzi." Na nilikuwa nikiwazia, usiku wa leo, juu ya kufanya mstari wa maombi wa mtindo wa kale, kama Ndugu Jack na Ndugu . . .

12 Ndugu Young Brown alikuwa akisambaza kadi za maombi kwa ajili yangu. Nami nilimwona kuwa ni mwaminifu sana wala kamwe sikuwahi kumshika akiuza kadi au akifanya kosa lolote, yeye ni mwaminifu sana. Na tumewashika wakijaribu kufanya hivyo, mwajua. Kwa hiyo—kwa hiyo sisi . . . Ndugu Young, alikuwa moja kwa moja kazini wakati wote, na mwaminifu. Na ninakumbuka, alikuwa akisimama na kuchukua kadi, na kuwapitisha kwenye mstari. Ningewaombea na wangepita mbele, watu hao walikuwa tu na hiyo imani isiyoghoshiwa, kama wangeweza tu kuja karibu na wewe wangeponywa. Na nafikiri kulikuwa na watu ishirini kwa mmoja walioponywa, ukilingansha na wale tulio nao sasa.

13 Halafu, hadithi hii ilikuja alasiri hii kumhusu mtu mmoja, yeye labda yuko hapa sasa. Kwamba alikuwa kwenye mstari wa maombi, mwaka mmoja uliopita, mahali fulani, na—na yeye alikuwa . . . kasema, katika utambuzi aliambiwa ya kwamba alikuwa amepatwa na matumbwitumbwi. Na madaktari walimwambia, baada ya matumbwitumbwi hayo kuondoka, ya kwamba asingeweza kuzaa mtoto msichana, naye daima alitamani mmoja. Nafikiri alikuwa na wavulana. Lakini katika ono lililotoka kwa Bwana, lilimwambia, "Lakini utampata mtoto huyo msichana."

14 Naye alisema ana msichana huyo mdogo hapa usiku wa leo. Simjui mtu huyo, huenda . . . je! ange—angeweza kuwa katika wasikilizaji, ama m—mtu ninayenena habari zake? Mahali fulani? Sijui, mtu fulani sasa hivi tu aliniambia habari zake, huko nje. Loo, huyu hapa mtoto huyo mchanga ametulia papa hapa, ameketi moja kwa moja pale. Hilo ni sawa. Hilo ni sawa kabisa. Ni maskini jamaa mzuri jinsi gani. Isingalikuwa mbali sana kumvuka kila mtu ili kuninii . . . katoto kachanga, kazuri sana, ningemwomba aje hapa na kutoa ushuhuda huo. Labda atautoa kesho, ama wakati mwingine tukiwa kwenye ibada zetu.

15 Sasa, kesho asubuni ni Kiamshakinywa cha Wafanyabiashara. Umetangaza jambo hilo, nafikiri? Na kwa hiyo hilo ni sawa.

16 Na sasa hebu na tupate ninii fupi—somo fupi juu ya uponyaji wa Kiungu. Ni wangapi wanaoamini katika jambo hilo? Loo, jamani, utakuwa usiku usio na kifani, mkiwa na imani kama hiyo. Watu wanaoamini, hilo ndilo linalohitajika. Ni kwa ajili ya waamini.

17 Sasa, basi, nilichukua penseli na kuanza kuandika somo fulani na kadhalika, na ninii . . . na ndipo Billy akabisha hodi mlangoni na kusema, "Baba?"

18 Nikasema, "Ngoja kidogo tu, bado sijamaliza."

19 Akasema, "Lakini, Ndugu Jack anakungojea." Kwa hiyo, i—ilinibidi kuja. Nikashikiza, sikuwa na kishikizo cha karatasi, nikachukua moja ya vipini vya Meda vya "kipolisi" ama namna fulani ya pini hapa wanazoita "chupio." Ilikuwa hizo, "chupio," namna fulani tu ya pini. Na—nami sijui mengi kuhusu vitu hivyo, mnajua, na niliiona tu imewekwa pale. Kwa hiyo, sasa ili kutengeneza kishikizo cha karatasi hapa, kutenga yale niliyokuwa . . . nilikuwa na mihitasari kwa ajili yake asubuhi; kuzitenga, kuzitenganisha.

20 Na ninapozidi kuzeeka . . . ilikuwa kwamba niliweza kwa urahisi kukumbuka hayo Maandiko na mambo kadha wa kadha kwa urahisi sana tu. Lakini, unajua, kwa namna fulani ni vigumu kufanya hivyo. Je! unapata shida hiyo, Ndugu Jack, bado? Hiyo ni kweli, naam. Nilimwambia Ndugu Jack, hapa si muda mrefu uliopita, nilisema, "Unajua, Ndugu Jack," nikasema, "ninafikia mahali ambapo siwezi kukumbuka." Nikasema, "Ninaanza kusema jambo fulani, na sina budi kungojea."

Akasema, "Huo—huo ndio umbali wote umeenda?"

Ndipo nikasema, "Vema, hivi huo si umbali wa kutosha?"

21 Akasema, "Hapana." Kasema, "Mimi ninampigia mtu simu halafu ninasema, 'Unataka nini?'" Nilifikiri ulikuwa ukinitania wakati ule, Ndugu Jack, nikaja kuona kwamba hilo ni kweli kabisa.

22 Naam, bwana. Jamani, jinsi mtu unavyosahau. Lakini hebu na tufanye mambo yetu yote sawa, kwa kuwa yamo katika kitabu fulani, kumbukumbu ambayo itachezwa kwenye siku ya hukumu.

23 Sasa, sisi ni kama familia moja kubwa. Na sidhani tumeunganishwa usiku wa leo, kote nchini, kama nilipokuwa nikihubiri ujumbe wangu jana usiku. Nafikiri labda ni kusanyiko tu la mahali hapa. Kwa hiyo, jana usiku, kwa kweli ninafurahia uungwana wenu wa kusimama . . . Mimi sijaribu . . . Sikujaribu kumshusha Ndugu Jack. Lakini yeye kila mara ameniambia, "Sema unalotaka kusema." Na kwa hiyo nimekuja tu hapa jukwaani na kuhubiri fundisho dogo. Lakini, kwa hiyo tunaninii tu . . . endapo baadhi ya ndugu zangu wa kimadhehebu.

24 Niliota ndoto, hivi majuzi asubuhi. Mimi mara nyingi sioti, mimi si mwotaji. Lakini ni—niliota ya kwamba nilimwona mtu, jamaa mmoja mdogo amefungwa pingu, alikuwa akijaribu

kutoka, nami nikasema...Mtu fulani aliniambia, akasema, "Hao ni watu wabaya sana, usijihusishe chochote nao."

25 Ndipo nikamwona jamaa huyu kijana akitoka kwenye pingu zake kwa hiyo nikamwacha tu. Nikawaza, "Nitaona tu atakalofanya." Kwa hiyo akatoka nje, naye alikuwa mtu mzuri. Baadaye nikaona wengine wakijaribu kutoka.

26 Sasa, hii ni ndoto tu. Basi nikaenda upande huu na nikamwona ndu—ndugu fulani, Roy Borders, rafiki yangu mpenzi sana, anayeishi California. Ilionekana kana kwamba alikuwa na shida fulani, macho yake yalikuwa yamefumbwa nusu, na ninii kubwa mno...labda kansa ama kitu fulani kwenye macho yake. Nami...mtu fulani alikuwa akijaribu kunivuta kutoka kwake. Nikapaza sauti, "Ndugu Borders! Katika Jina la Bwana Yesu, toka katika hilo!"

27 Naye ilikuwa ni shida kwake kuzungumza, akisema, "Ndugu Branham, itahitaji kitu fulani zaidi ya hiki. Siwezi kabisa kulipata jambo hilo, Ndugu Branham. Siwezi kabisa kulielewa."

28 Nikasema, "Loo Ndugu Borders." Ninampenda.

29 Basi mtu fulani akanivuta nikaondoka, ndipo nikaangalia, na ilikuwa ni bibi fulani aliyekuwa amesimama hapa. Ninii... nilipokuwa mvulana mdogo, ni—nilikuwa nikibeba bidhaa za vyakula kutoka kwenye masoko ya vyakula kuwapelekea watu. Na jina lake lilikuwa ni Bibi Fenton, angali anaishi Jeffersonville, rafiki yetu mimi na mke wangu.

30 Naye akasema, "Ndugu Branham, tutoe hapa." Kasema, "Hii ni nyumba ya kuzimu." Kisha kasema, "Umeeleweka vibaya." Na kasema, "Hawa...Pia wewe uliwaelewa vibaya watu hawa, hali kadhalika." Kasema, "Hawa ni watu wazuri, lakini..." Nami nikaangalia kule, na ilikuwa kama ghala kubwa mno iliyo chini ya ardhi, ama—ama kuta kubwa, chini ya pango kubwa; na nguzo kubwa za chuma, unene wa inchi nane ama kumi. Na watu, wamerukwa na akili, mikono na miguu iliyonyongwanyongwa, wakigongagonga vichwa vyao namna *hiyo*. Naye alikuwa analia, akisema, "Waokoe hao watu, Ndugu Branham." Kasema—kasema, "Tusaidie, tuko katika shida." Yeye mwenyewe, ninamjua, yeye ni mfuasi wa...Ninaamini ni kanisa la Kristo, ama kanisa la Kikristo, linaloitwa Kanisa la Ndugu. Kwa hiyo yeye...

31 Nikaangalia pande zote, kisha nikasema, "Laiti ningaliweza." Na nikaendelea, nikiangalia pande zote; nami... maskini mwili wangu mdogo sana na—na hizo ninii kubwa, nguzo kubwa mno za chuma; na maskini watu hao wakiwa mle ndani. Wala hungeweza kuwafikia, hizo nguzo za chuma zilikuwa zimekaa karibu-karibu. Basi nikaangalia, nao walikuwa wakijigonga vichwa vyao kana kwamba walikuwa wamerukwa na akili.

32 Kisha nikaona nuru fulani ikimulika mle ndani. Ndipo nikaangalia juu, na Bwana Yesu alikuwa amesimama hapo amezungukwa na nu—nu—nuru za upinde wa mvua. Alikuwa akiniangalia moja kwa moja, kasema, "Waokoe hao watu." Ndipo akaenda zake.

33 Basi nikawaza, "Vema, ningewezaje kuwaokoa? Si—sina nguvu za kutosha mikononi mwangu kuzivunja nguzo hizo."

34 Kwa hiyo nikasema, "Ewe nyumba ya kuzimu, vunjika katika Jina la Yesu Kristo."

35 Na milio yote ya mikwaruzo ya vyuma na vishindo, na—na miamba ikifingirika, na—na nguzo zikianguka; na watu wakikimbia, wakipiga makelele, "Tumekombolewa!" na kupiga makelele kwa sauti zao zote, na wote wakakombolewa.

36 Nami nilikuwa nikipaza sauti wakati huo, "Ndugu Roy Borders, uko wapi? Uko wapi? Mungu anawakomboa watu Wake! Uko wapi, Ndugu Borders?" Nimeshangaa kuhusu jambo hilo.

37 Mnajua, Ndugu Borders anaogopa sana. Mnajua ule unabii, nyote. . . wengi wenu mnajua, mnachukua kanda na kadhalika, kuhusu Pwani ya Magharibi.

38 Wako watu wanaoketi papa hapa, usiku wa leo, waliokuwa pale wakati jambo hilo lilipotukia (wakati tulipokuwa tumesimama pale, kwenye ziara ya kuwinda), mhudumu fulani aliyekuwa anasikiliza jana usiku. Akiwa na jicho lililopofuka, alikuja tu pale na kusema . . . akajitambulisha. Alikuwa amevaa miwani ya rangi, huko juu mlimani. Akasema, "Ndugu Branham," kasema, "Mimi ni Ndugu McHughes." Akasema, "Ni—nilisaidia kudhamini mmoja wa mikutano yako wakati mmoja, huko California."

39 Nikasema, "Ninafurahi kukufahamu, Ndugu McHughes."

40 Kwa hiyo kulikuwa na watu kama ishirini waliosimama pale. Tulikuwa tumetoka kwenda kuwinda ngiri. Ndipo nikasema, siku moja kabla ya kwenda mlimani, nilimwambia Ndugu Banks Wood . . . Nyote mnamjua, rafiki wangu msiri. Nikasema, "Ndugu Wood, . . . " Nikaokota jiwe na kulitupa juu hewani, na likarudi chini. Kisha nikasema, "BWANA ASEMA HIVI, jambo fulani liko karibu kutukia."

41 Kwa hiyo, akasema, "Ni kitu gani, Ndugu Branham?"

42 Nikasema, "Sijui, lakini katika saa ishirini na nne mtaona. Jambo fulani liko karibu kutukia. Ambalo ni ishara kubwa."

43 Na kesho yake . . . hiyo ilikuwa ni alasiri moja ya jioni iliyoenda sana. Kesho yake, kama saa nne, tulikuwa tukijiandaa kuondoka. Kila mtu alikuwa na ngiri wake, nasi tulikuwa tumesimama pale. Na Ndugu McAnally, mwajua, na hao wote, walikuwa wakiwatengeneza, na—na mimi na Ndugu Borders; na Ndugu Roy Roberson, shujaa wa vita aliyehasirika, rafiki

wangu mpenzi, wa thamani sana, naye alikuwa amesimama pale. Ndipo nikaangalia juu, ndipo Ndugu McHughes akasema, “Ndugu Branham, je! Malaika wa Bwana huwa anakutokea wakati ukiwa kwenye safari hizi za kuwinda?”

44 Nikasema, “Ndugu McHughes, ndio. Hiyo ni kweli. Lakini, ninakuja huku nipate kupumzika kwa namna fulani.”

45 Akasema, “Vema, Ndugu Branham,” kasema, “Sikutaka kukusumbua.”

46 Nikasema, “Hukunisumbua.”

47 Ndipo mara nikaangalia pande zote, na nikamwona daktari mmoja akiliangalia jicho lake. Sasa, mimi sikumjua, alikuwa amevaa miwani nyeusi, ambapo kuna mwanga mkali sana na jua kali huko Arizona. Nami nikaliangalia, na nikamwona daktari akimwambia, akisema, “Bwana, nimekuwa nikitibu jicho hilo kwa miaka kadhaa, miaka miwili, kitu kama hicho.” Kasema, “Mzio ulio nao jichoni mwako, utapoteza jicho lako. Unakula kuingia kwenye sehemu ya kuona, wala hakuna njia niwezayo kuuzuia.”

48 Kisha nikasema, “Sababu ya wewe kuniuliza jambo hilo, ni kwa sababu ya jicho lako. Miwani hiyo ni kwa sababu tu una jicho bovu.”

49 Akasema, “Hiyo ni kweli.”

50 Nikasema, “Daktari wako,” (nikatoa wasifu wake) “alikwambia, siku chache zilizopita, ya kwamba ‘Utapoteza jicho hilo kwa sababu huo—huo mziro unakula kwenye sehemu za kuona za jicho hilo.’ Naye amekuwa akilitibu kwa miaka kadha, wala hawezi kuuzuia.”

51 Akasema, “Ndugu Branham, hiyo ni kweli.”

52 Ndipo nikaanza kugeuka na kuangalia, nami nikamwona mwa—mwanamke mwenye umri mkubwa zaidi sana kuliko yeye, mweusi kidogo. Asili yao ni mahali fulani huku Arkansas. Na kwa hiyo akapandisha sketi ya—ya—yake na kumwonyesha mwanawe mguu wake, na kusema, “Mwanangu, kama ukimwona Ndugu Branham, mwambie aombe kwa ajili ya miguu yangu.” Naye alikuwa na vivimbe virefu vilivyoning’inia kati ya vidole vyake na kadhalika.

53 Nikasema, “Mama yako ni mwanamke mwenye mvi, naye alipandisha sketi yake, akashusha stokingi za—zake na akakuonyesha miguu yake, na kukwambia kama ukiniona uniambie nimwombee.”

54 Naye akasema, “Loo, mama wee.”

55 Nikaangalia nyuma na kumwona amesimama pale bila miwani, ono, nikasema, “BWANA ASEMA HIVI, Mungu aliponya jicho lako, na amemponya mama yako, pia.”

56 Yapata wakati huo, nikageuka . . . Sasa, kuna mtu anayeketi hapa, aliyekuwa amesimama pale. Nikamwambia Ndugu Roy Borders . . . ama Ndugu Roy Roberson, nikaweka mkono wangu juu ya bega lake, kwa kuwa yeye ni shujaa wa vita mstaafu, nikasema, "Ndugu Roy, ingia chini ya kitu fulani, upesi sana, jambo fulani liko karibu kutukia."

57 Akasema, "Unamaanisha nini, Ndugu Branham?"

58 Nikasema, "Usizungumze! Ingia chini ya kitu fulani, upesi!" Ndipo nikageuka na kuchukua sepetu, pale karibu na mahali hapo, na kuwaondokea maana nilijua itakuja mahali nilipokuwa.

59 Moja kwa moja karibu na lile genge kuu, refu mara nane ama kumi kuliko jengo hili, ni genge lililo kama "kasha"; kama moto ukishuka kutoka Mbinguni, kama upepo wa kisulisuli, futi chache tu juu ya mahali nilipokuwa nimesimama. Na ukalipua miamba moja kwa moja kutoka kwenye mlima, ukatoka ukaenda na kukata vilele vya miti ya vichaka, urefu wa yadi mia moja. Kila mtu akikimbia, na kujaribu kuingia chini ya magari na chochote kile. Ulirudi juu tena na kutoa sauti ya ngurumo kubwa. Ukarudi mbinguni tena, kisha ukashuka tena. Ulifanya hivyo mara tatu. Na wakati yote yalipokwisha, wao walikuja na kuuliza, "Hiyo ilimaanisha nini?"

60 Nikasema, "Sitaki kuwaambia; ilikuwa ni ishara ya hukumu. Katika siku chache, tetemeko kuu la ardhi litapiga upande wa Magharibi. Wala halitazuilika. California, Los Angeles itazama. Inazama. Itateleza moja kwa moja iingie baharini." Na siku mbili baadaye, tetemeko la Alaska liliitikisa Alaska.

61 Na halafu basi, ule mkutano wa mwisho niliokuwa nao huko California, nilipokuwa nikizungumza, wala sikujua jambo lolote lilitukia mpaka nilipofika barabarani, California iliambiwa, kasema—kasema, "Kapernaumu, Kapernaumu, mji unaoitwa kwa jina la malaika," (huo ni Los Angeles) "umejiinua hata mbinguni, lakini utashushwa hata kuzimu. Kwa kuwa kama ile miujiza mikubwa ingalifanyika Sodoma iliyofanyika kwako, ungekuwa umesimama hata siku hii."

62 Sasa, siku chache zilizopita, ile ngurumo ya kutisha na kulipuka. Halafu, hapa linatokea gazeti la sayansi, likasema, "Yote ni mashimo-mashimo kama sega, lazima izame." Wao wanajua jambo hilo kabisa.

63 Nanyi angalieni, maji yatarudi nyuma moja kwa moja mpaka kwenye Bahari ya Salton. Los Angeles imehukumiwa kuangamizwa. Ninawaambia kabla halijatukia, ili mjue wakati litakapotukia. Sikusema jambo hilo hata kidogo kwa nafsi yangu. Wala hajawahi kamwe kuniambia jambo lolote isipokuwa lile lililotukia. Nanyi mnaweza kushuhudia jambo hilo. Hiyo ni kweli. Lini? Sijui.

64 Nilitoka, nao wakaniambia niliyosema. Nami nikasikiliza, nikarudi na kuyachunguza Maandiko. Mwajua, Yesu alisema, karibu katika maneno yayo hayo, juu ya Kapernaumu; na Sodoma na Gomora ilikuwa—ilikuwa chini ya Bahari ya Chumvi, nadhani wakati huo ndipo ilikuwa imezama. Na baadaye, kama miaka mia moja baadaye, Kapernaumu ilididimia baharini, na iko baharini. Mungu yeye yule aliyeizamisha Sodoma baharini kwa ajili ya dhambi zake, Mungu yeye yule aliyeizamisha Kapernaumu baharini kwa ajili ya dhambi zake, Mungu yeye yule ataizamisha Los Angeles baharini kwa ajili ya dhambi zake, jiji hilo la—la upotovu.

65 Ndugu Roy Borders ameogopa nusura kufa. Sijui iwapo kuninii . . . kama hilo linamaanisha hilo, ama ni nini. Sijui.

Na tuombe.

66 Bwana, ni vema sana kushuhudia kwa wasikilizaji halisi. Tunaamini, Bwana, saidia kutokuamini kwetu. Nasi tunatambua ya kwamba tunashuka moja kwa moja kwenye mwisho wa ulimwengu. Kwamba ni wakati gani, hatujui. Lakini huko kutwaliwa kwa siri kwa Bibi-arusi; moja ya siku hizi, Bwana, tuta—tutanyakuliwa, tutanyakuliwa kwenda juu pamoja Naye. Nasi tunaingojea siku hiyo. Itayarishe mioyo yetu, Bwana.

67 Wako wengi. Tunaangalia, waliolala hapa kwenye vitanda vidogo na machela, wanaume na wanawake ambao wamefungwa na yule adui. Wapo watu walioketi kule, labda, usipowagusa, watakufa kwa mishtuko ya moyo. Labda baadhi yao wameliwa na kansa.

68 Na Baba, Wewe unajua moyo wa kila mtu. Unaujua kama ni mnyofu ama si mnyofu. Nasi tunasema mambo haya kwa sababu tunajua yale Wewe uliyofanya, nguvu Zako kuu zimewakomboa wengi. Sisi ni mashahidi wa hayo, ingawa wanajaribu kutuambia ya kwamba "mambo hayo hayatendeki." Lakini yanatendeka Bwana. Sisi ni mashahidi.

69 Ninaomba usiku wa leo, Bwana, ya kwamba kwa namna fulani utajenga imani katika mioyo ya watu hawa, hivi kwamba kila mmoja wao atakombolewa, watu hawa wote walio wagonjwa na wanaoteseka. Na liwe ni jambo rahisi sana, Bwana, tujalie tu, tunapojaribu kulifundisha Neno. Roho Mtakatifu na achukue makosa yangu, Bwana, na kuyasahihisha katika mioyo ya watu. Na aufanye kuwa usiku halisi, halisi sana hata ninii . . . hata Yeye aweze kujifanyia Mwenyewe makao katika moyo wa kila mwamini hapa. Tumeutenga usiku huu kwa kusudi hilo, Bwana. Jalia wale ambao hawajaokolewa, zaidi ya yote, wawe tayari; wajitayarishe sasa, wakati milango ya Rehema ingali inafunguliwa. Tunaomba hili katika Jina la Yesu. Amina.

70 Sasa tutafungua Maandiko, kwanza, na katika . . .

71 Mtu fulani aliweka mu—muhtasari mfupi hapa kwenye dawati, na kusema wao "wamechukua sadaka" kwa ajili

yangu usiku wa leo. Hilo halikuwa la lazima, msifanye hivyo. Siwezi kuirudisha. Ninakumbuka wakati mmoja, huko Calgary, Canada, tulichukua sa-. . .sadaka hii ilichukuliwa. Ndugu Jack alikuwa akijaribu kuniambia. . .Mke wangu akiwa ameketi huko nyuma; yeye, watoto walikuwa na vyumba viwili vya kizamani tulimokuwa tukiishi, ilimbidi kuweka blanketi mlangoni kufunga m—mlango ili watoto wasipate nimonia. Naye akasema. . .Akaniambia, kasema, "Ndugu Branham, hivyo si vizuri kumfanyia mkeo." Kwa hiyo, mnakumbuka kisa hicho. Walichukua, ninasahau ni dola elfu ngapi.

72 Nami nikasema, "Loo, zirudisheni, Ndugu Jack."

73 Akasema, "Sasa, tutazirudisha namna gani?" Kwa hiyo, niliinunua nyumba hiyo na ipo pale. Kwa hiyo, kwa ajili ya utukufu na heshima ya Mungu. Tuliiweka kwa miaka kadhaa, mimi na mke wangu, kama zawadi ya watu kutoka kwa kanisa.

74 Halafu basi nikawazia, "Hilo halisikiki sawa. Sikuleta kitu katika ulimwengu huu, ni dhahiri kwamba sitaondoka na kitu." Kwa hiyo nikaghairi na kuipeana, nikaikabidhi rasmi kwa maskani. Ili kwamba nitakapoondoka, mbona, mtumishi mwingine wa Mungu, kama ikiwepo kesho, ataitumia wakati huo. Unaona? Kwa hiyo, asanteni sana, wapendwa. Mungu na awabariki, kwa ajili ya jambo hilo.

75 Sasa, katika Yakobo, Kitabu cha Yakobo, mlango wa 2. Tunataka kusoma, kuanzia kwenye kifungu cha 21.

76 Na sasa, niko karibu. . .Muda mfupi wa kufundisha, na ndipo tutaanza kuwaombea wagonjwa upesi tuwezavyo, na kuwapitisha watu wengi sana katika mstari huu wa maombi kadiri tuwezavyo. Na hebu tuninii, pia, tumkumbuke pia. . . Sitaki kumsahau Dada Anna Jean na Ndugu Don, na hao wengine, nadhani wako mahali fulani huko Thailand. Sivyo? Kuelekea wapi? Bangkok, na—na maeneo ya mishenari. Kuna mambo mengi sana unayowazia mchana, unayotaka kuyataja mbele za watu. Halafu wakati unapokuja hapa, hu—huwezi kuyakumbuka, unaendelea moja kwa moja na somo hilo.

77 Na sasa, katika Yakobo hapa, sura ya 2. Nasi tutaanzia kwenye kifungu cha 21 cha mlango wa 2 wa Yakobo Mtakatifu, na kusoma se—sehemu Yake. Kifungu cha 21 cha mlango wa 2.

> *Je! baba yetu Ibrahimu hakuhesabiwa kuwa ana haki kwa matendo, hapo alipomtoa Isaka mwanawe juu ya* ninii. . .*ya madhabahu?*
>
> *Waona kwamba imani ilitenda kazi pamoja na matendo yake, na ya kwamba kazi*. . .imani *ile ilikamilishwa kwa njia ya matendo yale?*
>
> *Maandiko yale yakatimizwa yaliyonena, Ibrahimu alimwamini Mungu, na ikahesabiwa kwake kuwa ni haki: naye aliitwa Rafiki ya Mungu.*

78 Sasa, somo langu usiku wa leo. . .Na shikilieni Biblia zenu sasa, maana nina Maandiko mengi yaliyoandikwa hapa. Kama hatutachukua muda mrefu sana, nitarejea kwenye mengi yao. Somo langu ni: *Kazi ni Imani Katika Matendo*. Sasa, kumbukeni: *Kazi ni Imani Katika Matendo*. Matendo yanaonyesha ya kwamba imani tayari imetia nanga, unaona. Unaona? Sasa, tulichagua hili kwa sababu sisi. . .Ninaamini ya kwamba huenda likatusaidia kuelewa. Sasa sikilizeni kwa makini sana, nasi tutaliendea kama somo la Shule ya Jumapili.

79 Hapa Yakobo anaeleza katika fundisho lake, kutoka katika Mwanzo 22:1-9, kile *mwanadamu* alichoona katika Ibrahimu.

80 Hebu na turudi tu nyuma, kwa namna fulani nimewekea alama Maandiko yaliyoandikwa hapa. Katika Mwanzo, mlango wa 22, na kifungu cha 1 hadi cha 9.

> *Ikawa baada ya mambo hayo, kwamba Mungu alimjaribu Ibrahimu, akamwambia, Ee* Abramu. . . *Ibrahimu! Naye akasema, Tazama, mimi hapa.*
>
> *Akasema, Umchukue sasa mwanao, mwana wako wa pekee, umpendaye, Isaka, ukaende zako mpaka nchi ya Moria; ukamtoe. . .sadaka ya kuteketezwa huko juu ya mlima mmojawapo nitakaokuambia.*

Unaona, Yeye hata hakumwambia ulikuwa ni upi. Wewe endelea tu Mungu anaponena, endelea tu mbele. Unaona?

> *Ibrahimu akaondoka alfajiri, na akatandika punda wake, na akachukua kijana wake wawili pamoja naye, na Isaka mwanawe, akachanja kuni kwa ajili ya hiyo sadaka ya kuteketezwa, akaondoka, akaenda mpaka mahali alipoambiwa na Mungu. . .alipoambiwa.*
>
> *Siku ya tatu Ibrahimu akainua macho yake, akapaona mahali pakali mbali* sana.
>
> *Ibrahimu akawaambia vijana wake, Kaeni ninyi hapa pamoja na punda; na mimi na kijana tutakwenda kule, tukaabudu, na kuwarudia tena.*

81 Sasa, alikuwa ameyakinia moyoni mwake sasa, atamuua mwanawe, maana Mungu alimwambia amuue. Lakini angalia Maandiko hapa.

> *. . .mimi na kijana tutakwenda kule, tukaabudu, na kuwarudia tena.* (Yeye pamoja *na* kijana.)
>
> *Ibrahimu akazitwaa kuni na hiyo sadaka ya kuteketezwa, akamtwika Isaka mwanawe; akatwaa moto na kisu mkononi mwake; wote* wawili. . . *wakaenda wote wawili pamoja.*
>
> *Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akinena, Babaangu: naye akasema, Mimi hapa, mwanangu.*

Akasema, Tazama! moto upo, na kuni zipo: lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa?

Ibrahimu akasema, Mwanangu, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka, mwanangu: basi wakaendelea wote wawili pamoja.

Wakafika mahali pale alipoambiwa na Mungu; Ibrahimu akajenga madhabahu huko, akaziweka tayari kuni, kisha akamfunga mwanawe*. . .Isaka mwanawe, akamweka juu ya madhabahu, juu ya zile kuni.*

Ibrahimu akanyosha mkono wake, akakitwaa kisu ili amchinje mwanawe.

Ndipo malaika wa Bwana akamwita kutoka mbinguni, akasema, Ibrahimu! Ibrahimu! Naye akasema, Mimi hapa.

Akasema, Usimnyoshee kijana mkono wako, wala usimtendee neno; kwa maana sasa ninajua ya kuwa unamcha Mungu, iwapo hukunizuilia mwanao, nanii wako*. . .kutoka kwangu. . .mwanao wa pekee.* (Ni tendo la namna gani!)

82 Sasa, tunaona hapa ya kwamba Yakobo anamhesabia haki Ibrahimu kwa matendo yake.

83 Lakini sasa, katika Paulo, katika Warumi, Kitabu cha Warumi, ninii wa 8. . .mlango wa 4, 4:1 hadi cha 8. Sipasomi pote, lakini nitasoma tu sehemu yake.

Basi, tusemeje juu ya Ibrahimu, baba yetu kwa jinsi ya mwili?

Kwa maana ikiwa Ibrahimu alihesabiwa haki. . . (Mnakumbuka, tulilichukua neno hilo jana usiku, "kuhesabiwa haki.")*. . .kwa ajili ya matendo yake, analo la kujisifia; lakini si mbele za Mungu.*

Maana maandiko yasemaje? Ibrahimu alimwamini Mungu, ikahesabiwa kwake kuwa haki.

Lakini kwa mtu afanyaye kazi, ujira wake hauhesabiwi kuwa ni neema, bali kuwa ni deni.

84 Sasa—sasa kile Paulo anachorejea hapa, ni kile *Mungu* alichoona katika Ibrahimu.

85 Sasa hebu. . .kama mkininii. . .kama hatufungui mengi mno, tungerudi nyuma tena katika Mwanzo, mlango wa 15, na kifungu cha 6; 15:6, ninaamini ni kweli. Tutaanzia kwenye cha 5.

Akamleta nje, akasema, Tazama sasa kuzielekea mbingu, *kazihesabu nyota, kama ukiweza kuzihesabu. Akamwambia, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.*

Akamwamini Bwana, naye akamhesabia jambo hili kuwa haki.

86 Sasa hao watu wawili waliokuwa wakinena juu ya imani: Paulo alimhesabia Ibrahimu haki kwa yale *Mungu* aliyoona katika Ibrahimu; lakini Yakobo alimhesabia Ibrahimu haki kwa yale *mwanadamu* aliyoona katika—katika Ibrahimu.

87 Unaona, sasa, Yakobo alisema, "Yeye anahesabiwa haki kwa matendo yake."

88 Paulo alisema, "Anahesabiwa haki kwa imani."

89 Lakini unaona, Ibrahimu alimwamini Mungu, hicho ndicho *Mungu* alichoona ndani yake; aliamini jambo Hilo. Lakini basi wakati alipoanza kutenda kana kwamba jambo hilo lilikuwa tayari limetimia, hayo ndiyo *mwanadamu* aliyoona ndani yake.

90 Na hivyo ndivyo ilivyo na kwetu sisi, kwa maana matendo yetu yanaonyesha imani tuliyo nayo. Lakini kama tunaogopa kutenda yale tunayoamini, basi hatuamini jambo Hilo. Unaona, huna budi kuamini jambo Hilo.

91 Kazi za Ibrahimu zilikuwa zikionyesha imani yake aliyokuwa nayo katika ahadi ya Mungu. Sasa, Ibrahimu, kumbukeni, alikuwa na umri wa miaka tisini . . . umri wa miaka mia moja, na Sara alikuwa na umri wa miaka tisini. Na sasa walikuwa wazee, wamepita umri wa kupata mtoto, walikuwa hivyo kwa miaka kadhaa wa kadhaa. Nao walikuwa wameishi pamoja kama mume na mke tangu walipokuwa watoto, wala hawakuwa na watoto. Lakini hata hivyo, Mungu alimwambia wakati alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, na Sara akiwa na sitini na mitano, "Utapata mtoto." Naye akaamini ahadi ya Mungu. Akaiamini. Sasa, unaona, alitayarisha kila kitu kwa ajili ya mtoto huyu. Unaona, hayo ndiyo *Mungu* aliyoona, wakati alipomwamini Mungu; na *mwanadamu* aliona kile alichofanya kuonyesha yale aliyoamini. (Na jambo lilo hilo ndilo linaloendelea usiku wa leo, vivyo hivyo ndivyo ilivyo kwetu sisi.) Imefunuliwa kwake. Unaona, ilikwisha kufunuliwa kwake, kwa hiyo akaliamini kuwa ni kweli, naye alikuwa akitenda kana kwamba tayari limekwisha kutukia.

92 Sasa, hebu na tusimame hapo tu, kwa dakika moja. Mara nyingi tunaelewa jambo hili vibaya. Watu hushikwa na mhemuko, nao wanajaribu kuishi kwa mhemuko. Hilo halitafaa kitu.

93 Sasa, mimi ni kama Ndugu Gerholtzer hapa, sisi—sisi ni wazee, na tumekuwa katika ninii . . . hii kwa muda mrefu, na tumeona uzuri na ubaya, na—na kila kitu. Na kuwaombea wagonjwa, kote ulimwenguni, na kuona ku—kuadhirika kwa watu, na kuona zile—zile "Haleluya" kutoka kila upande. Basi, yote haya, tunajifunza kwayo. Sasa, wakati tulipokuwa wavulana, na tukaanza kuhubiri hili, Ndugu Gerholzer, kama vile tulivyoanza kuogelea. Jambo la kwanza, unajua, ilikuwa kwamba ningetoka, na ningeninii . . . Ndugu Jack, ilibidi Ndugu Brown anizungushe mtaani, usiku baada ya usiku, kujaribu

kunifanya nijirudie. Ningesimama pale, kama mtoto mdogo, anayepiga maji, nikiona maono, unajua. Nami ningekaa tu pale mpaka Ndugu Brown . . .

94 Ninakumbuka usiku mmoja, sitausahau kamwe, huko San Jose ama mahali fulani. Alikuja kuniamsha, sikuwa nimelala kwa siku kadhaa wala sikujua nilikuwa nikizungumza na mtu huyo, lakini alisema nilimwambia. Nikaanza kulia, nikasema, "Ninaenda nyumbani." Unaona?

95 "Mbona," akasema, "huwezi kwenda nyumbani. Kuna mkutano unaoendelea kule chini."

96 Nikasema, "Vema, nitakuwa niko tayari katika dakika chache kwenda nyumbani." Unaona, niko mbali, karibu sijitambui. Unaona, nilikuwa mvulana wakati huo.

97 Kama vile wakati unajifunza kuogelea, unajua, unarusha maji na kuvuka kidimbwi, huyoo "hwaa, hwaa, hwaa, nimefaulu!" Sasa, baada ya kujifunza kuogelea, mkambi unakuwa wa madaha zaidi, wala "haukuchoshi" sana. Unaona, ndivyo ilivyo, unajifunza jinsi ya kufanya jambo hilo; na kukata kila kona na kulifanya vizuri zaidi, na hilo linakuwa ni rahisi zaidi. Unaona?

98 Mvulana mdogo ambaye hajawahi kutembea, akijaribu kutembea kwenye marefu haya ya kanisa hapa, angeanguka mara dazani na "kuchoka" kabla hajafika pale. Lakini mtu yeyote anayejua jinsi ya kutembea, mwanariadha, angetembea moja kwa moja kwenye marefu hayo ya kanisa na wala hata asijisikie ametembea. Vema, ilimbidi kuanza namna hiyo, hivyo ndivyo alivyo sasa.

99 Vema, hivyo ndivyo ilivyo katika kuhubiri uponyaji wa Kiungu ama chochote kile. Unaposonga mbele, unaanza kujifunza. Kama hujifunzi, kuna kasoro fulani. Unaona, huna budi kujifunza, na huna budi kujifunza jinsi ya kumkubali Mungu na maana yake hasa.

100 Tunaliruhusu, wakati mwingine twasema, "Vema, mtu huyu hakuwa na imani ya kutosha, mtu huyu hakufanya jambo *hili* na *hili*." Kuna sababu hapo kwa ajili ya jambo hilo, kuna sababu. Wakati mwingine ni dhambi isiyotubiwa. Ungeweza kumwagia mtu galoni ya mafuta, na kupiga makelele mpaka upwelewe na sauti, haitatikisa pepo huyo kamwe. La, bwana! Huna budi kutubia jambo hilo. Hivyo ndivyo utambuzi unavyofanya, kusema, "Nenda ukaweke sawa jambo hilo, ondoa jambo hilo."

101 Lakini linaenda pole pole sana kufanya hivyo, unaona. Halafu basi—halafu hao wengine wanakosa subira, na kusema, "A-ha, mimi sikuombewa kabisa." Lakini tunataka kupata njia sasa, ambayo . . . kile kinachotukia, msingi halisi wa uponyaji wa Kiungu.

102 Sasa, karama, kama tu nilivyosema jana usiku, "Karama ni nzuri sana, lakini huwezi kuweka kikomo chako cha Milele juu ya karama." Huwezi kujijengea msingi wako katika jambo lililo dogo, na ka—karama ni jambo dogo. Na Shetani anaweza kuigiza karama yoyote aliyo nayo Mungu, anaweza kufanya kitu kinachofanana kabisa nayo, unaona, kinachofanana kabisa. Kwa hiyo, hatuna budi kuwa macho na jambo hilo.

103 Kama vile wakati mwingine mimi ninavyosema juu ya kupiga makelele; nimeona pepo wakipiga makelele, mnaona. Kunena kwa lugha, nimeona pepo wakinena kwa lugha. Hakika, yeye huiga Hilo. Si kitu cha kweli, lakini anaigiza Hilo, unaona, anaifanya ionekane kana kwamba ni kitu halisi. Na watu wakati mwingine, ambao hawajui tofauti yake, wanatangaza kwamba *hii* ni "halisi" wakati si halisi.

104 Nao wanafanya jambo lile lile kuhusu uponyaji wa Kiungu. Wanafikiri, "Vema, ni udanganyifu, ama kitu kama hicho." Sivyo. Ni imani ya kweli, isiyoghoshiwa katika yale Mungu aliyosema kwamba ni Kweli. Na hilo linatia nanga! Na linapotia nanga, hakuna kitu kitakachoitikisa. Itakaa pale. Na kwa hiyo, kukata kona hizi, . . .

105 Sasa, *imani* ni "ufunuo kutoka kwa Mungu." Sasa, imani ni ufunuo. Hapo ndipo ninapotaka kukaa, hapo, kwa muda kidogo tu. Ni ufunuo. Yeye amekufunulia jambo fulani kwa neema Yake. Hakuna kitu ulichofanya. Hukujitahidi upate imani. Kama ukiwahi kuwa na imani, umepewa hiyo kwa neema ya Mungu. Na Mungu anakufunulia, kwa hiyo imani ni ufunuo. Na Kanisa lote la Mungu limejengwa juu ya ufunuo.

106 Mhudumu wa Kibaptisti aliniambia, si muda mrefu uliopita, alisema, "Siwezi kamwe kukubali ufunuo."

107 Nikasema, "Basi huwezi kukubali Biblia. Huwezi kumkubali Kristo, kwa sababu Yeye ni Ufunuo wa Mungu. Yeye ni Mungu aliyefunuliwa katika mwili." Kwa hiyo, Kanisa lote limejengwa juu ya ufunuo wa Kiungu.

108 Yesu alimwambia (ninaamini ilikuwa ni Petro). . .kasema, alisema, "Watu wanasema kwamba Mimi Mwana wa adamu ni nani?"

109 Alikuwa akisema na wanafunzi Wake. "Na wengine walisema Wewe ni 'Eliya,' na 'Musa,' ama 'Mmojawapo wa manabii,' na 'Yeremia.'"

110 Yeye akasema, "Lakini ninyi mnasema mimi ni nani?"

111 Akasema, "Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai."

112 Sasa, kanisa la Katoliki ya Kirumi husema, "Alikuwa akimwambia Petro, 'Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa langu.'"

113 Waprotestanti walisema, "Alikuwa akilijenga juu ya nafsi Yake."

114 Sasa, huenda wawe sahihi. Lakini, kwangu mimi, wote wawili wamekosea. Ilikuwa ni juu ya ufunuo wa kiroho wa kwamba Yeye alikuwa nani. "Mwili na damu havikukufunulia jambo hili, Petro. Bali Baba Yangu, aliye Mbinguni, amekufunulia jambo hili. Na juu ya mwamba huu," ufunuo wa kile Yeye alichokuwa; juu ya ufunuo huo: Yeye ni Neno, na lote... "Juu ya mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu, na milango ya kuzimu haiwezi kulishinda." Ilionyesha milango ya kuzimu ingelipinga.

115 Habili, kwa imani, ufunuo, (pasipo Biblia iliyokuwa imeandikwa katika siku hizo), kwa...Habili, kwa imani, alimtolea Mungu dhabihu iliyokubalika kuliko ile ya Kaini. Ambayo Mungu alishuhudia, "Yeye alikuwa mwenye haki." Vipi? Kwa imani. Vipi? Kwa ufunuo! Kwa ufunuo, Habili alimtolea Mungu dhabihu iliyo bora zaidi, kwa maana ilifunuliwa kwake ya kwamba haikuwa ni matunda ya kondeni, ilikuwa damu.

116 Hiyo ndiyo sababu watu wengine wanaweza kuamini jambo Hilo, na wengine hawawezi kuliamini, wengine wanajaribu kujifanya wanaliamini.

117 Katika hadhara ya watu, ambapo mstari wa maombi unapita, utaona baadhi...na wote walikuwa watu wazuri, tuseme. Kuna wengine wanaokazana kwa bidii sana kuliamini, wakijaribu kuliamini. Wengine hawawezi kuliamini hata kidogo. Na wengine, ni kwa neema tu, wanapewa bure tu. Sasa, hiyo ndiyo tofauti. Unaona? Inatendeka hivyo. Huo ndio ufunuo halisi, kwa maana imani ni ufunuo kutoka kwa Mungu. Haina budi kufunuliwa kwanza.

118 Yesu alisema jambo hili dhahiri aliposema, "Hakuna mtu anayeweza kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza, ama kunifunua Mimi kwake kwanza." Unapaswa kusoma jambo hilo. Liko katika Yakobo Mt.... ama Yohana Mt. 6:44 na mpaka 46. Wao hawakujua Yeye alikuwa nani. Walidhani alikuwa ni mtu wa kawaida tu. Walimdhania kuwa tu, kama watu wanavyodhania leo, nabii fulani. Yeye alikuwa Nabii, alikuwa mtu wa kawaida, lakini kulikuwa na zaidi ya hayo.

119 Ni kama tu jana usiku, nikizungumza...Utakapopata kile kitabu, labda utaona kuchanganyikiwa kudogo pale kwa yale niliyosema, "Vile vitabu viwili vya Uzima." Ni Kitabu kile kile, lakini kimoja cha hivyo ni kuzaliwa kwako kwa asili, hicho kingine ni kuzaliwa kwako kiroho. Kimoja kinaongoza kwenye hicho kingine, kama vile tu shina la ngano. Vema, sasa, kila unapozungumza na mimi, unazungumza kunihusu mimi kama mtu aliye hai. Lakini kuna sehemu yangu hapa, ndiye mtu huyo, ambaye hana budi kuangamia. Hicho ndicho kile Kitabu ambamo jina linafutwa. Lakini yule wa Milele, yule Aliyechaguliwa Tangu Zamani, yule Aliyeteuliwa, jina hilo haliwezi kamwe kuondolewa kwa sababu daima lilikuwa

limeandikwa Humo. Haliwezi kuondolewa kamwe. Utaona hilo katika kile kitabu, kwa hiyo kuchanganyikiwa kwako kutakwisha. Utakuta jambo hilo hivyo. Kwa sababu, nafikiri, Ndugu Vayle, aliyekitia sarufi sahihi, alinikumbusha jambo hilo leo. Nikasema, "Hilo ni sawa."

120 Wabatisti wanaamini kuna vitabu viwili mbalimbali. Na kwa njia moja ni vitabu viwili mbalimbali, na katika njia nyingine si vitabu viwili mbalimbali. Mimi ni watu wawili mbalimbali...Mimi ni mwili na nafsi na roho, watu watatu mbalimbali, lakini mimi...ni mwili mmoja tu unaonifanya mimi mtu.

121 Kuna Kitabu kimoja tu halisi cha Uzima. Kama vile kulivyokuwa na chembechembe moja ya—ya ngano iliyokua kupitia kwenye shina, na kupitia kwenye kishada, na kupitia kwenye ganda, na kuingia katika ngano; kotekote kupitia pale, unasema, "Sasa, hiyo ni ngano iliyo pale." Si ngano, ni shina, lakini yote kwa pamoja ni ngano. Unaona, ni ngano kwa sababu yote ni shina moja, lakini ngano ndiyo unayonena habari zake, ile punje juu kileleni. Hizo nyingine zilikuwa ni bebaji, hazina budi kutoweka. Na hiyo ndiyo sehemu—mahali pamoja inaposikika kana kwamba jina lako linaweza kuondolewa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, na hapo pahali pengine huwezi kufanya hivyo. Kwa hiyo, hivyo ndivyo ilivyo. Yote yamo kwenye huo ufunuo mkuu pale, ambao ulijulikana katika wakati wa ile Mihuri Saba. Kwamba ni kwa nini, ni imekuwaje watu wengine hawawezi kuamini jambo Hilo?

122 Yesu alisema ya kwamba "Hakuna mtu anayeweza kuja Kwangu asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba, watakuja Kwangu." Hakuna mtu anayeweza kufahamu kwamba Yeye ni nani, ama jinsi Hilo lilivyo, isipokuwa lifunuliwe kwako na ufunuo wa Mungu. Na ndipo imani katika jambo hilo, unatenda vilivyo. Unaona? Hapa tunaona dhahiri ya kwamba Mungu amefunuliwa katika Yesu, na ni wale tu waliokusudiwa tangu zamani kuliona, wataliona. Hakikisha kusoma Maandiko haya, niliyaacha wakati huo, hayo ya Yohana Mt. 6:44 mpaka 46. Niliyaacha kwa sababu nilifikiri labda tungekuwa...labda hatutakuwa na wakati wa kutosha wa kuyapitia, kwa sababu ile saa kule inazidi kusonga mbele tu.

123 Na kwa hiyo sisi...Unaona, "Hakuna mtu, hakuna mtu anayeweza kuja asipovutwa na Baba Yangu kwanza. Na wote alionipa Baba, watakuja." Wataliona jambo Hilo. Hakuna mtu mwingine anayeweza kuliona jambo hilo, hakuna mtu mwingine, hata awe mzuri namna gani, hata uwe nani, halina budi kufunuliwa kwako. Ndipo unamwona Yesu Kristo ni nani.

124 Sasa, hapa, mpango uliokusudiwa tangu zamani unaonekana wazi. Kama vile tu mbegu nyingine, Neno la Mungu ni Mbegu na halina budi kutayarishiwa shamba kwanza. Kama

ulipanda mbegu, ukazitupa tu kule shambani, hazingefaa kitu, ndege wangezidonoa. Ukizitupa kati ya michongoma na miiba, itazisonga upesi sana. Mfano wa Yesu ulisema hivyo. Kwa hiyo shamba halina budi kutayarishwa kwanza. Kwa hiyo, Mungu, katika neema kuu, huutayarisha moyo kwanza. Yeye alikuandaa kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kumpokea katika wakati huu. Alitangulia kukujua kwa kujua Kwake tangu zamani, na akakuchagua upate Uzima wa Milele. Alikujua, kwa hiyo Yeye akakutayarisha.

125 Hiyo ndiyo sababu uliyumbayumba ukatoka kwenye mambo haya, na ukayumbayumba ukaingia mahali ulipo sasa. Ilikuwa ni Mungu akikuongoza kwenda mahali ambapo Yeye alikuchagulia kuwa. Ninii. . . ama kama—kama—kama shamba hili halikuandaliwa awali ya yote, haliwezi kukua. Hiyo ndiyo sababu, mbegu ya imani, unapohubiri imani, unaona utambuzi wa Bwana, na kuona jambo linalotukia, na karama zote za Biblia zikifanya kazi. Watu wanajichochea, "Loo, haleluya, ninaamini," kisha wanakuja, na kujikuta wameadhirika. Unaona, shamba hilo halina budi kuchaguliwa tangu zamani. Na mtu unajua wakati Hiyo inaingia moyoni.

126 Kama vile kinda wangu wa tai, jana usiku. Alijua wakati aliposikia mlio huo wa huyo mama tai, "kuna tofauti kubwa sana kati ya huo na mlio wa kuku." Unaona, kwa sababu yeye alikuwa tai toka kwenye yai. Si. . . yeye hakufanywa tai wakati huo huo, alikuwa tai sikuzote. Na Mkristo sikuzote alikuwa hivyo! Hiyo ndiyo sababu, talaka, wakati ulipotaliki, kwa sababu ulikuwa umenaswa katika jambo hilo, unaona, na mzazi wako wa kwanza, Adamu na Hawa. Ukawa kwa asili ni mwenye dhambi. Hukutaka kuwa hivyo, lakini basi ulisikia Injili, na "imani chanzo chake ni kusikia," ufunuo huja kwa kusikia. Kuna kitu fulani kidogo ndani yako.

127 Mtu mwingine anayeketi karibu kabisa na wewe, anasema, "Aha, siamini takataka hizo. Upuuzi! Siamini hayo. Hakuna lolote!"

128 Kama vile walivyofanya katika ile Siku ya Pentekoste, walicheka na kusema, "Watu hawa wamejaa divai mpya." Wanajua ilikuwa ninii. . . Lilikuwa jambo kubwa kwa hao ambao lilikuwa likiwatukia. Kwa nini? Ilikuwa ni Mungu akijifunua Mwenyewe kwa watu binafsi. Wakati wengine walicheka, hawa walikuwa wakishangilia. Ilikuwa ni ufunuo wa mtu binafsi, ambao imani; imani iliyofunuliwa. Kama haikuwa ni imani, basi hata haingalikuwapo. Ilikuwa imani.

129 Mbegu tu ndizo ambazo hazina budi kuandaliwa shamba kwanza. "Kwa hiyo, wote aliotangulia kuwajua, aliwaita. Wote aliowaita. . . Wote aliotangulia kuwajua, aliwachagua tangu zamani." Ukitaka kusoma hayo, Warumi 8:28-34, na pia Waefeso 1:1-5. Unaona, wote aliotangulia kuwajua, aliwaita.

Wote aliowaita, aliwahesabia haki. Na wote aliowahesabia haki, amewatukuza tayari. Hakuna kitu kilicho nje ya utaratibu. Tunafikiri kipo, lakini angalia katika Maandiko. Inatimia vile vile hasa Neno la Mungu lilivyosema yatatimia. Tunaona Ujumbe umekataliwa, leo. Je! hivyo sivyo hasa Maandiko yalivyosema wangefanya? Hakika, mambo haya yote yameamuriwa na Mungu.

130 Loo, linapaswa kukufanya utembee kwa furaha. Hiyo ndiyo shida yetu leo, tofauti kubwa sana na Wakristo wa kale. Wakati ule ufunuo halisi, wa kweli wa Yesu Kristo kuwa ni Imanueli ulipokuwa ndani ya mioyo ya watu hao, walikuwa watu jasiri. Lakini siku hizi tunabembelezwa na madhehebu, na "Loo, nakwaambia, hao hawana Ufunuo. Wewe njoo huku." Unategemea ufunuo *wao*. Kama ufunuo wao haulingani na Neno la Mungu, basi si wa kweli; wangu ama wa mtu yeyote yule, hapo ndipo ukweli wa mambo unapotokea. Neno la Mungu linatwambia lipi ni la kweli na lipi ni la uongo!

131 Mbegu yoyote haina budi kuwa na shamba lake, bila shaka. "Kwa hiyo, wote aliotangulia kuwajua . . . " Unaona, tayari alijua jambo ambalo lingetendeka. Angalia, Yesu alisema tena, kuhusu hiyo Mbegu, "Nyingine zilianguka juu ya mwamba, nyingine katika ardhi ya mchanganyiko." Unaona, mahali palipokuwa na michongoma, miiba, na chochote kile, haingeweza kukua. Na nyingine kwenye ardhi nzuri, ardhi nzuri, udongo mzuri, uliokuwa umekwisha kutayarishwa, umetayarishwa tayari.

132 Watu wote hapa, mtu ni kama kuku, anatafutatafuta, akijaribu kupata. Anapata *hiki*, na anapata *kile*, lakini baada ya kitambo kidogo unakuja Mlio wa ghafla kutoka Mbinguni. Anautambua mara moja, "Hilo ni Neno la Mungu!" Unaona, anaujua kwa sababu kuna kitu fulani moyoni mwake ambacho ameambiwa, kimefunuliwa kuhusu kitu Hicho.

133 Angalia, nabii Isaya alisema, "Bikira atachukua mimba." Ni msemo wa kushangaza jinsi gani. Jinsi m—mtu aliye na akili zake timamu angeweza kusema jambo hilo? Hapajapata kuwa na bikira aliyechukua mimba. "Bikira atachukua mimba!" Sasa, yeye hakuona wasiwasi kuhusu kusema jambo Hilo, alilisema tu. Atazaaje? Vema, hilo halimhusu! Yeye . . . Ni kusema tu yale Mungu aliyosema yatatendeka. Mungu alimfunulia jambo hilo, alimwonyesha ono; akamfunulia, na lilikuwa ni la kweli.

134 Ni Mungu yeye yule tu aliyeniambia mtoto huyo mchanga angezaliwa na mtu huyo ambaye hangeweza kumzaa mtoto, ama kuzaa msichana. Kama hayo mengine na kadhalika, jinsi linavyosikika la kushangaza wakati daktari anaposema, "Haliwezekani!"

135 Lakini Mungu anaposema, "Itatendeka," inategemea ni neno la namna gani linaloingia ndani. Kumbuka, nabii alisimama pale na Neno Lake likatoka.

136 Kama vile Mungu, katika Mwanzo 1, Yeye alisema, "Na iwe nuru. Na *hiki* kiwepo. Na *kile* kiwepo." Akaumba mtu kwa mfano Wake, kwa mfano wa Mungu aliwaumba, mwanamume na mwanamke, na hapakuwa na kitu duniani bado. Halafu, tunaona katika Mwanzo 2, hapa, Yeye alimwumba mtu katika mfano Wake. Hapakuwa na mtu wa kuilima ardhi, baada ya huo uumbaji mwingine. Ilikuwa ni nini? Ni Maneno Yake, alikuwa akilinena. Na wakati aliponena, Yeye alisema, "Iwe nuru." Huenda hakukuwa na nuru kwa miaka mia nane baadaye, huenda hakukuwa na nuru, lakini Yeye aliitamka! Na mradi tu alitamka jambo Hilo, "Na kuwe na mtende. Na kuwe na mwaloni. Na kuwe na *hiki*," hizo mbegu zilikuwa zikiumbika chini ya maji hayo. Hiyo ni kweli. Na katika majira yake, katika wakati wake, katika msimu wake, ilizaa! Haliwezi kushindwa, ni Neno la Mungu. Haliwezi kushindwa hata kidogo. Limekwisha kutamkwa.

137 Sasa, siku moja, Mungu alizungumza na mwanadamu, uso kwa uso. Lakini katika wakati wa Musa, wakati ule moto ulipokuwa ukishuka, wao walisema, "Acha Mungu... Acha Musa anene; si Mungu, tusije tukaangamia."

138 Kwa hiyo, Yeye akasema, "Sitanena nao namna hiyo tena. Nitawainulia nabii." Hivyo ndivyo utaratibu wa Mungu ulivyokuwa sikuzote.

139 Sasa, huyu hapa nabii amesimama; sasa, yeye yuko chini ya upako; yeye hafikirii juu ya elimu yake, "Sasa, ngoja kidogo. Kama ningesema hivyo, vema, unajua, watu wangefikiri mimi ni kichaa." Unaona, hiyo ni akili yake; hapo anamsikiliza Shetani, kama vile tu Hawa alivyofanya.

140 Na mradi tu daktari anasema kwamba "Huwezi kuishi. Huwezi kuwa mzima. Huwezi kufanya *hivi* ama *vile*." Mradi tu unasikiliza jambo hilo, Mbegu hiyo haitaanguka kamwe katika shamba kama hilo na kufanya jambo lolote jema. Haiwezi. Lakini wakati jambo fulani linaporarua hayo yote, na inaanguka katika ardhi hiyo yenye rotuba, hakuna kitu kinachoweza kuirarua.

141 Sasa, haidhuru litachukua muda gani, litatukia. Sasa, Yeye alisema, "Bikira atachukua mimba." Je! ulijua ilikuwa ni miaka mia nane kabla jambo hilo halijatukia? Mungu alimjua mwanamke huyo tangu zamani, kwamba atakuwa nani, kwamba jina lake lilikuwa nani, mahali ambapo Mbegu hiyo ingeangukia. Unaamini jambo hilo? Hakika, alijua! Na kutoka kwenye tumbo la uzazi la kibinadamu kungetokea muujiza huu mkuu. Mungu alijua kuhusu jambo hilo, Yeye alilifunua tu kwa nabii Wake aliyekuwa mwaminifu na akalinena Neno. Bila hata ya kuwazia kwamba ilikuwa ni kitu gani, yeye alilitamka tu. Hakujaribu kulihoji.

142 Kama ukijaribu kuhoji. . . Vipi kama mtu huyu, mwanamke huyu, ama mwanamume huyu anayeketi hapa, ama mtu fulani akijaribu kuhoji, "Sasa, nimekuwa kiwete miaka hii yote. Daktari anasema, 'Hakuna uwezekano wowote'"? Vema, kadiri ajuavyo yeye huenda kusiweko, na hiyo ni kweli.

143 Lakini kama kitu fulani kinaweza kung'oa hayo magugu, kama Mungu kwa neema Yake; si mhubiri, si mtu mwingine. Lakini Mungu anaweza kuweka moyoni mwako ufunuo fulani, ya kwamba, "Mimi nitakuwa mzima," hakuna kitu kitakachokufanya ukae pale. Hakuna kitu kinachoweza kukushikilia pale, utakuwa mzima! Lakini mpaka jambo hilo litukie, utakaa pale pale ambapo daktari anasema utakaa; mpaka jambo hilo litukie. Halina budi kufunuliwa. Neema ya Mungu ndiyo inayofunua jambo hilo.

144 Sasa, angalia, Mungu alijua mwanamke atakayejiliwa na jambo Hilo. Angalia Isaya, hapakuwa na swali. Isaya hakusema, "Ngoja kidogo, Bwana! Hebu. . . Hebu kidogo tu! Uliniambiaje, ati 'Bikira atachukua mimba'? Vema, sasa, sasa ngoja, Baba, ha—ha—hapajakuwa na kitu kama hicho kilichopata kutendeka."

145 Hakusitasita, yeye alisema tu, "Bikira atachukua mimba!" Vema.

146 Mwangalie Mariamu: "Sasa, sasa Bwana, ngoja kidogo. Unajua kamwe si—sijamjua mwanamume. Hii haiwezekani! Hakuna jambo kama hili lililopata kutokea! Salalaa, loo, la, hakuna jambo kama hili lililopata kutokea. Nitampataje mtoto huyu? Simjui mwanamume yeyote, kwa hiyo haiwezekani! A-ha, ewe Malaika, umekosea tu. Nimepatwa na mazingaombwe. Unajua, kanisa langu linasema, 'Siku hizi zimekwisha.'" La! Haingeweza kuangukia mahali kama hapo. Mariamu hakuhoji.

147 Alisema, "Inawezekanaje? Simjui mwanamume."

148 Akasema, "Roho Mtakatifu atakutia uvuli. Hivyo ndivyo itakavyotukia."

149 Akasema, "Tazama, mimi ni mjakazi wa Bwana!" Hakuna swali!

150 Unaona, Isaya, wakati Mungu alipoleta Neno kwa wazo (ufunuo) katika moyo wa Isaya, liliangukia kwenye ardhi nzuri, ilikuwa ni nabii. Nabii huyo hakujali hekima ya mtu yeyote. Hakujali kusoma kwa mtu yeyote. Hakujali umaarufu wa mtu yeyote. Alikuwa ni njia iliyowekwa wakfu kwa Mungu, ndipo Mungu akanena naye akanena. Hivyo tu. Kama liliudhi, kama halikuudhi; kama lilisikika la kiwenda wazimu, kama halikusikika la kiwenda wazimu; haikuleta tofauti yoyote kwake. Ilikuwa ni Mungu, si mtu huyo.

151 Na wakati Neno hilo lilipotamkwa, sasa Hilo linakuwa Mbegu, halina budi kuangukia mahali fulani. Kama Mungu alinena jambo Hilo, hapana budi pawe na tumbo la uzazi mahali

fulani ambapo Hilo litaangukia. Kama tu Yeye alivyosema, "Mambo yote yanawezekana kwao waaminio. Kama ukiuambia mlima huu, 'Ng'oka,' wala usitie shaka moyoni mwako, yatakuwa yako." Unaona, hapana budi kuwepo na mahali palipo sahihi!

152 Hebu angalia! Sasa, tunaona ya kwamba Isaya hapa alinena habari Hiyo.

153 Bikira Mariamu, mara . . . Shamba lilikuwa limelimwa tayari. Alikuwa bikira. Hakuwa "amezurura." Shamba hilo lilikuwa tayari limetayarishwa, ama kuchaguliwa tangu zamani kwa kutangulia kujua kwa Mungu.

154 Hata alisema, "Yeye alikuwa bikira." Papo hapo Mungu alijua jina lake lingekuwa nani. Jina lake lilikuwa katika Kitabu cha Uzima Mbinguni.

155 Basi, lilithibitishwa. Mwanadamu basi (kwa mwanadamu) aliona onyesho Lake kwa matendo, wakati lilipokuwa limefanyika tayari. Sasa tunaangalia nyuma na kusema, "Hakika, lilikuwa limetendeka," maana tunaona kazi zilizofanywa.

156 Matendo ya Nuhu yalidhihirisha kwa mwanadamu, jinsi imani yake katika ahadi ya Mungu ilivyokuwa. Sasa, Mungu alikutana na Nuhu, Na akasema, "Nuhu, itanyesha. Nitaiangamiza dunia nzima kwa maji." Sasa, haikuwa kamwe imenyesha, hilo lilikuwa ni jambo lisilowezekana. Vema, sasa, Nuhu alipata . . . Kasema, "Jenga safina ya vipimo nitakavyokwambia." Naye akiwa seremala, basi akaanza kazi na akaanza kuchukua tezo yake, na kila kitu cha kukatia mbao, na kuijenga pale kwa mbao za mshita, na kuifunika kwa lami kama tu Yeye alivyosema. Basi unawazia vile watu walivyowazia juu ya mtu huyo?

157 Wao walisema, "Mtu huyo kweli ana kichaa, kwa maana anasema, 'Maji yatatoka mbinguni,' wala hakuna maji huko juu." Lakini, unaona, Nuhu hakuwazia juu ya jambo hilo. Kazi zake zilikuwa zikiwaonyesha watu jinsi imani yake ilivyokuwa na yale Mungu aliyosema yangetukia.

158 Hiyo ndiyo sababu Mkristo halisi hujitenga na kila kitu ila Neno la Mungu, haidhuru watu wanafikirije, mtu yeyote anavyosema. Yeye ametengwa kwa sababu . . . Yeye hasemi jambo hilo kwa kulisema tu; kama anafanya hivyo, haitachukua muda mrefu hata matendo yake kufichuka. Yeye atarudi nyuma na kwenda *hivi*, na kujiunga na *hili* na *hili*. Na aanze . . . A— ataonyesha jinsi alivyo. Lakini kama yeye ni mnyofu, kama Neno la Mungu limekaa ndani yake, basi litazaa kwa jinsi Yake, utamwona mtu huyo akijiandaa kwa ajili ya ile saa kuu. Unaona, hivyo ndivyo Nuhu alivyofanya.

159 Musa, akiwa na fimbo mkononi mwake, alikuja kuwatoa watu toka kwa Farao. Sasa, ungeweza kuwazia . . . Musa, Biblia

ilisema ya kwamba alikuwa ameelimishwa katika hekima yote ya Wamisri. Yeye alikuwa mwerevu, aliweza kufundisha mambo yao ya kielimu. Alifundishwa hekima yao yote. Haikumbidi kuongezea elimu yake. Sasa, wazia tu juu ya mtu fulani huko jangwani, akiwa na elimu hiyo yote, halafu Mungu anamtokea na kusema, "Musa, chukua fimbo hii mkononi mwako ushuke uende huko Misri, ukawatoe watoto wangu kwa ufito huu ulio nao mkononi mwako. Charaza tu kitu hicho chote kwa ufito huu."

160 Sasa, vipi kama Musa angalisema, "Bwana, hebu kidogo, nilidhania nilikuwa nikizungumza na Kiumbe chenye akili, huyu 'MIMI NIKO' mkuu ambaye unasema huyo ni Wewe. Sasa, ninawezaje kamwe kuchukua maskini fimbo hii ndogo ya kale iliyopindika, niliyo nayo hapa mkononi mwangu, na kushinda jeshi la wanaume milioni, wenye mikuki, wapiganaji? Wala mimi si mpiganaji, mimi ni mchungaji. Ningewezaje kufanya jambo hilo?"

161 Hapakuwa na swali! Kwa nini? Kwa nini? Ile ardhi iliyo moyoni mwake! Alikuwa ni mtu aliyechaguliwa tangu zamani. "Karama na miito haina majuto." Mungu alikuwa amemwambia Ibrahimu ya kwamba Yeye angefanya hivyo, na hiyo hapo ardhi iliyoandaliwa tayari.

162 Ndipo Musa akachukua fimbo hii akashuka akaenda kule na kutoa taifa hilo kutoka kwenye taifa. Wakati alipokuja akiwa na fimbo mkononi mwake, na kumwambia Farao, "Waachilie waende!" Farao aliona hizo kazi ndani ya Musa, kwamba alikuwa na imani katika yale aliyokuwa atafanya, ama aliyokuwa akijaribu kufanya. Alikuwa na imani katika ahadi ya Mungu aliyetoa ahadi hiyo, akashuka kwenda kuiteka. Hakuna mtu mwingine angefanya jambo hilo, wala hakuna mtu mwingine angeliweza kufanya jambo hilo, yeye alikuwa amechaguliwa kufanya hivyo. Mungu, hapo nyuma, alikuwa amemwambia Ibrahimu ya kwamba hilo ndilo tu lingetendeka hasa. Na wakati wa ile ahadi ulipokaribia, mvulana mdogo alizaliwa, mtoto mzuri. Na wazazi wake, Amramu na Yokebedi, hawakuogopa amri ya mfalme. Mnaona, kulikuwa na kitu fulani, ardhi ilikuwa imeandaliwa tayari.

163 Ee Mungu, ninatumaini ninazungumzia ardhi iliyoandaliwa, usiku wa leo! Kama Mbegu inaweza kuanguka katika mahali pazuri, na itakuwa ninii . . . Kama sivyo, halitatukia.

164 Hilo ndilo jambo lile lile. "Mbona," unasema, "Ndugu Branham, hilo kwa namna fulani linatutoa sisi nje." Kama likiwatoa, linauondoa Ukristo, pia. Unaona, unaweza kuiga chochote. Lakini kama ninii . . . Kama kweli likianguka ndani, Neno la Mungu likianguka katika ardhi nzuri, litazaa kwa jinsi Yake. Halina budi kufanya hivyo, kwa maana Hilo ni Mbegu.

165 Nuhu . . . Musa, kazi zake, zilionyesha imani katika ahadi ya Mungu aliyemwamini. Farao, binadamu, aliweza kuona

ilikuwa ni nini. Si. . .asingeweza kuona vile Musa angefanya jambo hilo, lakini alijua Musa aliamini kile alichokuwa akinena habari zake la sivyo asingekuwa akisimama katika jumba la mfalme pale ameshika fimbo mkononi mwake. Kasema, "Kwa fimbo hii, nitawatoa kwako." Mzee, mwenye umri wa miaka themanini, si mwanariadha; mzee, mabega yaliyoinama, na masharubu yakining'inia kufikia kwenye ninii yake. . .labda kiunoni mwake; na nywele zenye mvi, endapo alikuwa na zozote. Na yuko pale ameshika fimbo mkononi mwake, akisema, "'Nitawatoa, achilia watu hawa waende,' BWANA ASEMA HIVI. Na usipofanya hivyo, Mungu atakuhukumu." Amina! Kwa nini? Hiyo ni. . .Unaona, inaninii. . .Je! yeye aliogopa? Mbona, mshale mmoja tu, mkuki mmoja, kitu kingine chochote kingemaliza jambo hilo. Alikuwa hana woga! Alijua barabara mahali alipokuwa amesimama; kasema, "Mungu atakupiga, ewe Farao." Naam, bwana.

166 Kwa kuwa Mungu alimwambia, "Utakuja kwenye mlima huu tena," naye alijua ataenda kule.

167 Haleluya! Tunajua tunakoenda pia, mwishoni mwa safari hii. Mungu ameahidi! Kuna Nchi iliyo ng'ambo ya mto. Uwe mjasiri katika ushuhuda wako. Amina. Kama jambo limefunuliwa kwako, wewe huna woga. Hujali kama ulimwengu mzima. . .yale wasemayo; huna woga. Wakati jambo linapofunuliwa kwako, "Hii ni Kweli inayotoka kwa Mungu," basi kuwa jasiri. La sivyo, huwezi kuwa mjasiri.

168 Daudi, akiwa na kombeo la mchungaji, alilionyesha jeshi lote la Israeli, imani aliyokuwa nayo katika Mungu wao. Sasa, kulikuwa na Goliathi upande ule mwingine, naye alisimama kule na kujigamba. Mkubwa mara nyingi kuliko Daudi, alikuwa na vidole vyenye urefu wa inchi kumi na nne. Naye alikuwa pandikizi la mtu, jamaa mkubwa mno, jitu la Kifilisti. Na huyu hapa Daudi, aliyekuwa mdogo kuliko wote, alikuwa mdogo mno kuwa jeshini; alikuwa amedumaa sana, hawangeweza kumtumia. Kwa hiyo, ndugu zake walikuwa wako huko nje jeshini. Na, halafu, Goliathi alikuwa akijigamba.

169 Lakini Daudi, sasa kumbukeni, ilifunuliwa kwa Daudi. Aliwazia, "Haya hapa majeshi ya Mungu aliye hai, yamesimama katika nchi yao wenyewe, na yule kule Mfilisti asiyetahiriwa anayejigamba." Tutamwita "kansa" usiku wa leo, tutamwita "mtu aliyepooza."

170 Mbona, Daudi hangethubutu kumkabili hata kidogo, si na silaha ya namna yoyote; hangemuweza. Mabega ya mtu huyo labda yalikuwa futi kumi, kumi na mbili upande mmoja hadi mwingine; labda alikuwa na urefu wa futi kumi na nne, kumi na tano. Mkuki kama mti wa mfumaji, labda urefu wa futi ishirini, ubapa wake labda ni wa futi nne upana.

171 Na maskini Daudi amesimama pale na kipande kidogo cha ngozi, ngozi ya mbuzi ama ngozi ya kondoo, kimefungiwa vipande viwili vya kamba. Lakini *ilifunuliwa* kwake! Ufunuo ulishuka juu yake! Amina! Akasema, "Mungu aliyenitoa kwenye makucha ya dubu, aliyenitoa kwenye makucha ya simba, ni zaidi jinsi gani atakavyomtoa Mfilisti huyo asiyetahiriwa mkononi mwangu!"

172 Ndugu zake, walikuwa na uwezo zaidi wa kufanya jambo hilo. Sauli, tangu mabega yake kwenda juu alikuwa mrefu kuliko jeshi lake. Lakini, unaona, haikufunuliwa kwao. Amina. Jambo ndilo hilo: waliamini lingeweza kutendeka, waliamini kwamba Mungu angeweza kufanya jambo hilo, lakini halikufunuliwa kwao; lakini ilifunuliwa kwa Daudi. Sasa, hiyo hapo tofauti yake, papo hapo. Kama imefunuliwa kwako kinaganaga ya kwamba Mungu atakuponya, uta—utapona. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Utapona. Sijali una shida gani, upinzani wa namna gani, huenda ukawa mbaya kuliko wa Daudi na Goliathi. Bali kama imefunuliwa kwako!

173 Pia angalia, ilipofunuliwa, Daudi akawa jasiri. Akasema, "Leo nitakikata kichwa chako!" Amina. Huyo ndiye Mungu wetu. Kwa neema, katika wakati huo wa hatari sana ambapo uamuzi ulipaswa kutolewa, Mungu yeye yule aliyetoa neema siku hiyo, na kuishusha hiyo mbegu ya imani katika mvulana huyo mwenye kuonekana ana kinundu, akiwa moyoni mwake; Mungu yeye yule, katika wakati huu muhimu, angeweza kumwondoa mwanamke yule kutoka katika kiti cha magurudumu, mwanamume *yule*; mwanamke *huyu* hapa; mtoto; ninii . . .? . . . Hiyo chembe ndogo ya imani inapofunuliwa kwako, basi sijali inachukua muda gani.

174 Sasa liangalie jitu hilo, likiwa upande ule mwingine, halikuamini; wala huyo kansa hataamini. Alicheka, akasema, "Hivi mimi ni mbwa? Ati mnamtuma mtoto huyo huku kupigana na mimi?" Kasema, "Nitakunyanyua, kwa ncha ya mkuki wangu, na kuwapa ndege waile nyama yako." Mbona, yeye alikuwa na ninii yote . . . yote, kila kitu upande wake.

175 Lakini, unaona, hilo halikumtikisa Daudi hata kidogo. Kwa nini? Ilifunuliwa kwake. Alikuwa na imani katika yale aliyokuwa akifanya. Alijua atafanya hivyo. Naye akafanya, ni kwa sababu ilifunuliwa kwake naye alijua mahali alipokuwa amesimama.

176 Na kama Mungu angalinena tu jambo hilo, moja kwa moja katika moyo wako usiku wa leo, awe amesema "Hutalala kwenye kitanda hicho. Hutaketi kwenye kiti hicho. Utakuwa mzima," hakuna kitu kingaliweza kubadilisha nia yako katika jambo hilo.

177 Lakini mpaka jambo hilo litakapotukia, kila mhubiri ulimwenguni angeweza kuomba, . . . sisemi hayangekusaidia;

yangekusaidia, yangekutia moyo. Lakini mpaka imani hiyo . . . Unaona, nguvu za uponyaji zimo ndani yako. Hazitoki kwa mhubiri. Zinakuja kwako kwa ufunuo, kwa imani. "Si kwa nguvu, wala si kwa uwezo, bali ni kwa Roho Yangu," asema Bwana. "Roho Wangu, kwa neema, anakufunulia jambo hili." Wala hakuna kitu kinachoweza kuuondoa. Kwa imani, ufunuo! Ndipo, Daudi kuthibitisha matendo yake, . . .

178 Sasa, baadhi yao walisema, "Ninajua wewe ni mtundu." Ndugu yake alisema, "Umekuja hapa kuona vita. Sasa, kimbia urudi walikokuwa hao kondoo."

179 Akasema, "Hebu nizungumze na Sauli, jemadari." Unaona?

180 Ndipo Sauli akasema, "Sasa, mwanangu, ninapendezwa na ujasiri wako, lakini, unaona, wewe si kitu ila kijana mbichi tu. Na yeye ni shujaa wa vita tangu utotoni, humuwezi."

181 Akasema, "Nilikuwa nikiwachunga kondoo wa baba yangu, . . ." Yeye angeweza kuliwekea msingi juu ya jambo fulani! Amina. Loo ndugu! Na Mungu yule aliyeiokoa nafsi yako, je! hawezi kuponya mwili wako? Ni jambo lile lile tu, kufunuliwa kwako, Yeye ni Mponyaji wako kama alivyokuwa Mwokozi wako. Unaona? Lakini haina budi kufunuliwa kwanza, hiyo ndiyo tofauti. Yeye alikuwa na kitu fulani cha kutegemeza imani yake.

182 Kasema, "Sasa, jambo hili halijawahi kutukia hapo awali."

183 Lakini akasema, "Mungu yeye yule aliyenikomboa na makucha ya simba, atanikomboa kutoka kwa yule Mfilisti asiyetahiriwa."

"Unajuaje, Daudi?"

"Ninaamini."

"Kwa nini?"

"Imefunuliwa kwangu." Naye akasema, . . .

184 Alijua alichokuwa akizungumzia. Kwa sababu wakati lile jitu liliposema, "Nitakulisha kwa ndege"; yeye alisema "Nitakikatilia mbali kichwa chako." Hiyo ndiyo tofauti yake, unaona. Naye alikikata!

185 Samsoni, alikutwa siku moja (amekosa ulinzi) mbugani, na hawa hapa Wafilisti elfu moja wanamjia. Ndipo akaangalia pande zote chini, na hapo ndipo nyumbu alikuwa amekufia, basi akaokota ninii, mfupa wa taya, uliokauka kwelikweli, akatimua mbio kuwaendea hao Wafilisti, akiwapiga kichwani kwa taya hili la zamani la nyumbu lililokauka, na nijuavyo mimi, hakuna hata jino moja lililong'oka toka kwalo. Na hizo helmeti za Wafilisti labda zilikuwa zina unene wa inchi moja (maana walipigana kwa marungu ya vita katika siku hizo), kumzuia mtu asiwapige kichwani. Lakini yeye aliitwaa taya la yule nyumbu na kuwapiga Wafilisti elfu moja, wala

hilo taya halikuvunjika. Aliendelea tu kuwapiga, namna *hiyo*, walipokuwa wakimjia. Kwa hiyo, hao wengine walikimbilia miambani, unaona, walikuwa wanamkimbia. Kwa nini? Yeye aliamini! Wakati mwingine . . . Hakika.

186 Ninataka kuwaambia jambo fulani sasa. Tenda kazi katika mdundo huo, kaa chonjo, kama alivyofanya Yoshua, kama Mariamu Magdalene, hao wote. Wakati huo huo tu jambo fulani linapofunuliwa kwako, linyakue. Lishikilie, kaa chonjo.

187 Naam, ilifunuliwa kwake. Aliondoka akaenda kukutana na hawa maelfu, ya Wafilisti. Sasa unafikirije wakati hao Wafilisiti waliposema, "Sasa, angalia, kile pale kinakuja, kile kiduva; chenye urefu wa kama futi nne na nusu tu, kwanza; akiwa na maskini vishungi vidogo saba vinavyoning'inia mgongoni mwake, kama maskini kidondoadume kipenzi cha mama yake, mnaona; kinakuja pale na taya la nyumbu. Hebu tuangalie, sisi ni jeshi kubwa jinsi gani! Hilo si ni dhihaka?" Lakini alikuwa akifanya nini? Alikuwa akiwaonyesha hao Wafilisti kile alichokuwa amefunuliwa na Mungu. Alinyakua hilo taya na kutimua mbio, kwa sababu hilo ndilo Yeye alilomwekea mkononi mwake; alimwekea hilo mkononi mwake, hivyo ndivyo alivyoamini: angeweza kutekeleza jambo hilo! Na kwa kufanya hivyo, alikuwa akiwaonyesha hao Wafilisti kile Mungu alichokuwa ameweka moyoni mwake kufanya.

188 Yohana Mbatizaji alionyesha imani yake kwa matendo yake, na wakati aliposema "Kuna Mtu anayesimama miongoni mwenu sasa." Hebu wazia tu jambo hilo. Yohana Mtakatifu, nina Andiko hilo, Yohana Mtakatifu 1:26, unaona. Yeye alisema . . .

189 Wao walisema, "Unasema, 'Ati Masihi yuaja'? Mbona," kasema, "jamani, hivi una nini? Tumekuwa tukimtazamia kwa miaka elfu nne."

190 Akasema, "Amesimama papo hapo miongoni mwenu sasa." Haleluya! Ndivyo alivyo usiku wa leo! A-ha.

191 Yeye alionyesha imani yake kwa ufunuo wake, kwa maana ilifunuliwa kwake ya kwamba . . . alijua angembatiza Masihi. Yeye alikuwa mtu, mwenye umri wa miaka thelathini. Alijua hana budi alikuwa yupo mahali fulani hapo; hakuwa amejua Yeye alikuwa nani, Naye alikuwa yupo hapo amesimama moja kwa moja miongoni mwao. Akasema, "Kuna Mtu mmoja anayesimama miongoni mwenu sasa, ambaye hamumjui, wala mimi sistahili kufungua gidamu za viatu Vyake, lakini Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu. Naye yuko papo hapo kati yenu sasa." Yeye aliionyesha, imani yake, kwa sababu alijua, katika siku zake, angemwona na kumbatiza Masihi wa Mungu. Kwa hiyo, mnaona, watu wangeweza kuona kwake onyesho hilo, katika njia aliyokuwa akihubiri na vile alivyokuwa akitenda, alikuwa akionyesha ya kwamba alikuwa na ufunuo wa kweli kutoka kwa Mungu.

192 Sasa, kuthibitisha ya kwamba ilikuwa ni kweli, moja kwa moja akaja Masihi akitokea kwenye kundi la watu; ni kijana mwanamume wa kawaida tu akitembea kule, amevaa kama watu wengine. Yohana akasema, “Tazama, huyo ndiye Mwana-Kondoo wa Mungu aichukuaye dhambi ya ulimwengu.”

193 “Unamjuaje?”

194 Akasema, “Yeye aliyeniambia, huko nyikani, ‘Mtu utakayeona akishukiwa na Roho, Huyo ndiye atakayebatiza kwa Roho Mtakatifu.’”

195 Unaona, alimjua kwa sababu kulipaswa kuwe na ishara mnamo wakati huo. (Mnalipata?) Yohana alijua wakati huo ulipokaribia, maana alikuwa nabii. Ilifunuliwa kwake, kwamba alijua mnamo wakati huo, angeona ishara. Na wakati alipoona ishara hiyo, alisema, “Yeye amesimama miongoni mwenu.” Alijua Yeye alikuwapo.

196 Loo, ninaona ishara ya kwamba wakati wa mwisho umewadia. Ninaona mambo yaliyoahidiwa, kwa ajili ya Ujumbe huu wa siku za mwisho, yakitimia (yakijitokeza) sawa kabisa na vile Maandiko yalivyosema. Nami ninajua ya kwamba wakati umekaribia! Ninasema hivyo bila kusitasita. Ninaamini ya kwamba umekaribia kabisa, kwa maana ninaona ishara alizosema zingetimia kabla tu ya wakati huo. Ziko tayari kutukia *sasa*.

197 Yohana alionyesha imani yake katika yale aliyokuwa amefunuliwa na Mungu. Kwa hiyo, matendo ni ushuhuda wa imani. Wanapokuona ukitenda kana kwamba umeponywa, basi watajua una imani ya kwamba umeponywa.

198 Ushuhuda unasema nini? Unasema hivi: “Ninalo sasa, kwa maana nimepokea ahadi ya Mungu. Sasa inafanya kazi ndani yangu. Ninajitayarisha kwa ajili ya hilo kutukia.” A-ha. Unaona, hivyo ndivyo unavyoshuhu-. . .kazi zako zinavyoshuhudia. Vema, hakika!

199 Hapa, hivi majuzi, baada ya ziara yangu iliyopita ya Afrika; nilikuwa tu kule majira haya ya kuchipusha majani, ukiacha ile ziara iliyotangulia hiyo. Kulikuwa na mtoto mchanga aliyekuwa na miguu iliyopindika, na mguu mmoja. . .mguu mmoja mfupi kuliko huo mwingine. Hajapata kuvaa viatu maishani mwake. Loo, alikuwa na ulemavu mbaya sana. Nami nikamwombea mtoto huyo mchanga usiku huo, walikuwa wameangalia na kuona mambo hayo yakitendeka, walimwombea mtoto huyo mchanga. Ndipo kesho yake asubuhi nikashuka nikaenda huko, nikapitia karibu na duka la viatu. Nikaingia mle, na huyo hapo yule mtu akimnunulia mtoto huyo jozi ya viatu vya kuvaa. Aliamini jambo hilo! A-ha.

200 Kama vile mtu huyu hapa, aliyeamini ya kwamba Mungu angempa mtoto huyo. Hakika, aliamini itatendeka, akajiandaa kwa ajili yake. “Ninajiandaa.” Ingawa hapakuwa na matokeo

ya maumbile ya mwili yaliyokwisha kuonekana, lakini hilo halikuleta tofauti hata kidogo. Aliamini, kama vile Ibrahimu, "akaita kila kitu kilichopinga kana kwamba hakikuweko." Hapo!

201 Kwa hiyo, kama akili yako ikikwambia, . . . Lo, huu hapa mwiba sasa. Kama akili yako ikikwambia ya kwamba "Hii ni Kweli, Mungu ni Mponyaji wa maradhi," moyo wako unaweza kushuhudia ya kwamba "Hiyo ni Kweli," lakini kama hakuna udongo wa kuzalia moyoni mwako (imani, mahali pa hilo kuangukia) kulifanya dhahiri, halitatukia. La. Kiasi . . .

Haidhuru mtu huyu wa nje anaweza kulihoji kiasi gani kwa Maandiko, na kusema, "ni kweli," hilo bado halilifanyi kuwa ni la kweli.

202 Ni wangapi wanaochukua kanda? Je! mlipata mahubiri yangu, si muda mrefu uliopita, *Watiwa Mafuta wa Siku ya Mwisho*? Mliamini hayo? Mnaona, ilisema, "Kutakuwa na wapinga Kristo. Wapinga kristo karibu watawapoteza walio wateule, kama yamkini." Inawezekana, pia? Haiwezekani, kwa sababu haiwezekani; wao wameteuliwa. Unaona? Vema.

203 Lakini Yeye alisema, "Watiwa mafuta." Unaona, *Kristo* maana yake ni "mtiwa mafuta," lakini hawa walikuwa ni wapinga. Walikuwa wametiwa mafuta, lakini ni wapinga, dhidi ya Kristo katika mafundisho yao. Sasa, wao wangeweza kufanya jambo lolote ambalo hao wengine wangefanya.

204 Sasa, kumbuka, wewe uko kwenye duara lenye sehemu tatu, bali wewe ni mtu mmoja. Kama vile Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu, duara lenye sehemu tatu, lakini ni Nafsi moja. Sifa tatu za Mungu yeye yule: ubaba . . . Ofisi tatu kama: ubaba, uwana, na Roho Mtakatifu. Nawe ni: mwili, roho, na nafsi.

205 Sasa, mwili wa nje una milango mitano ya kuingilia ndani, kuwasiliana na makazi yako ya duniani: kuona, kuonja, kugusa, kunusa, na kusikia. Ile ya ndani, ambayo ni roho, ina hisi tano: dhamira, na upendo, na kadhalika. Lakini ndani yake, nafsi, ina kitu kimoja. Hapo ndipo unapoishi *wewe*.

206 Roho anaweza kuja hapa na kukupaka mafuta ufanye mambo fulani, na unayafanya, lakini jambo hilo halimaanishi ya kwamba umeokolewa. Wazia jambo hilo. Kayafa alitabiri. Yuda alitoa pepo. Unaona, Roho alimtia mafuta. Mvua hii huwanyea wenye haki na wasio haki, magugu yanaweza kufurahi pamoja na ngano. Lakini ni kile kilicho kwenye kiini chake. Hapo ndipo ambapo ninyi wenye bongo mnapoweza kukubali jambo kiakili na kusema, "Loo, hakika, hilo linaonekana sawa. Ninaamini jambo hilo." Hilo bado halifai kitu. La, bwana. Na roho kweli anaweza kushuhudia jambo hilo, na bado lisiwe hivyo. Kwa kuwa kama nafsi hiyo haijatoka kwa Mungu, inaweza kufanya maigizo yote huku nje, lakini haiwezi kuwa halisi. Unaweza kuigiza kuponywa, unaweza kujifanya kama

umeponywa. Unaweza kujifanya kama kwamba umeupokea. Wakristo wanaweza kujifanya kana kwamba wao ni Wakristo, na waigize na wafanye jambo hilo vizuri sana, bali hilo halimaanishi ya kwamba wameokolewa. Hiyo ni kweli kabisa, unaona. Roho anaweza kuwa hapo, Roho halisi, wa kweli. Roho Mtakatifu anaweza kukutia mafuta, hilo bado halimaanishi umeokolewa. Ni hiyo nafsi ya ndani isiyoweza kufa, ina Uzima wa Milele. Daima ilikuwa ni Uzima wa Milele. Unaona? Inatoka kwa Mungu, inaenda kwa Mungu, ni nafsi.

207 Sasa, angalia hilo, halina budi kuwa. Tano, i-m-a-n-i, nje; roho, J-e-s-u-s (Yesu); upande wa ndani, y-o-u (wewe). Unaona? Hivyo ndivyo ambavyo nikisimama hapa, nikiwaangalia, simjui hata mmoja wenu. Roho anaweza kunipaka mafuta, ningali sijui hata mmoja wenu. Lakini wakati hiyo ndani ya ndani inapofunguka, huyo ni Mungu.

208 Hapo ndipo huku nje kunavyoweza kuhoji. Hebu mchukue mtu, useme, "Vema, unajua, na—najua sipaswi kufanya uzinzi. Lakini, unajua, ndipo roho ananiambia sipaswi kufanya uzinzi. Lakini, unaona, kule ndani kabisa kungali kuna kile kitu mle ndani." Unaona, kwa namna fulani kitatawala, na afadhali ukichungeze.

209 Lakini wakati kinapoongozwa kutoka ndani, kinavitupa hivyo vingine vyote pamoja. Hiyo ndiyo nguzo ya kuongozea. Huo ndio mnara wa kuongozea, kule ndani ya ndani. Nafsi huongoza roho, roho inaongoza mwili.

210 Kwa hiyo kupakwa chokaa kwa nje hakubadilishi chochote. Hao watu wa kidini kule nyuma, ambao Paulo aliwaita "kuta zilizopakwa chokaa," na kadhalika, walikuwa (kwa nje) kwa kila namna ninii . . . mwamini, nao walikuwa na unabii kati yao, na chochote kile ila kule *ndani ya ndani* ("ile *nafsi* isiyoamini").

211 Hiyo ndiyo sababu ninasema watu wanaweza kurukaruka, na kunena kwa lugha, watu wanaweza kupaza sauti, kuweka mikono yao juu ya wagonjwa, na kuwaponya wagonjwa na kadhalika, kwa imani; mambo haya yote makubwa pale kwa Roho, hata hivyo wapotee. Watiwa mafuta.

212 Angalia Yesu amesema, "Amini tu, kwa kuwa mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio." Imani na matendo ni mume na mke, vinafanya kazi pamoja. Mume hufanya kazi pamoja na mkewe, mke na mumewe; wanatambulishana.

213 Kama vile mtu akisema "ameoa" na hata hivyo hawezi kuonyesha wala kuthibitisha ya kwamba ana mke, unatilia shaka dai lake. Unaona? Mtu fulani alisema, "Nimeoa."

"Yuko wapi mke wako?"

"Loo, loo, si—sijui kuhusu jambo *hilo*." Unaona? Unaona? Kwa namna fulani itakuwa ni vigumu kwangu kumwamini.

Ninasema, "Vema, yuko wapi mkeo?"

"Vema, sijui." Si—sitaamini jambo hilo.

214 Kwa hiyo, unaona, kama una kile unachosema kwamba unacho, "Nina imani," utanionyeshaje kwamba una imani? Kwa matendo yako. Unaona?

"Nimeoa."

"Ninajuaje umeoa?"

"Huyu ndiye mke wangu." Unaona? Haya basi.

"Nimeolewa, huyu ndiye mume wangu."

"Nimeponywa."

"Unajuaje?"

215 "Matendo yangu yanaonyesha imani yangu." Unaona? Unaona? Sasa, kile—kile unachozungumzia: imani yako ndicho kitu Mungu anachoona ndani yako, matendo yako ndiyo watu wengine wanayoona ndani yako.

216 Hiyo ndiyo tofauti kati ya Yakobo na Paulo hapa, wakielezea juu ya Ibrahimu. Wao hawakuhitilafiana hata kidogo, wote walikuwa sawa; wameungana.

217 Vivyo hivyo na imani isiyoonyesha matendo, mtu yeyote ana haki ya kushuku ushuhuda wako. Sasa mmeyasikia hayo, kabla hatujaanza mstari wa maombi? Kama imani yako haizai kazi kwa matendo yake, huwezi kumfanya mtu yeyote aamini ya kwamba umeponywa. Unasema, "Vema, sijui." Unaona? "Mbona, naam, hakika, nina imani yote iliyopo duniani." Huna. Kwa sababu, kama unayo, una imani, basi matendo yameolewa na imani. Hao ni mume na mke, mmoja—mmoja humtambulisha huyo mwingine.

218 Hebu tufikirie juu ya Ibrahimu kwa dakika chache tu. Ibrahimu aliweka huo muungano mtakatifu katika ukamilifu, unaona, alileta kitu hicho chote pamoja. Aliviita vitu, vilivyo kinyume cha imani yake, kana kwamba havikuwapo; na akatumia kanuni ile ile. Ninaweza kuwazia, baada ya kama miaka ishirini, mtu fulani alipita kule na kusema, "Ati baba wa mataifa? A-ha! Abramu, ulisema ati ulisema jina lako lilikuwa ni *'Ibrahimu,'* ambalo maana yake ni *baba wa mataifa*. Hivi una watoto wangapi sasa hivi, Ibrahimu?" Unaona?

219 Hilo halikumfanya asitesite hata kidogo. Biblia ilisema, "Hakusita-sita kwenye Neno la Mungu, kwa kutokuamini." Aliendelea kujiandaa moja kwa moja, akitayarisha vijiatu vya mtoto na na vitundu na kila kitu, yeye "atazaa mtoto." Hivyo tu.

220 Hata Sara alisema, "Unajua litakalotukia? Utapata mtoto, lakini hebu nikwambie jinsi tutakavyompata. Hajiri sasa ni mjakazi wangu, nitakupa wewe." Maana, mitala ilikuwa halali wakati huo. "Naye atazaa mwana, nami nitamchukua mtoto huyo." Lakini Ibrahimu hakuamini jambo hilo. La, asingefanya hivyo. Lakini Sara alivuviwa kufanya jambo hilo.

221 Kwa hiyo, Mungu akamwambia Ibrahimu, “Endelea na umsikilize,” lakini Yeye akasema, “hata hivyo hivi sivyo nilivyokuahidi. Hivi sivyo nilivyoliahidi.”

222 Sasa angalia, aliita chochote kwamba ni “kinyume,” na mwili wake umekufa wakati huo, na tumbo la uzazi la Sara vile vile. Sasa, yeye alikuwa mzee, mwenye umri wa miaka mia moja. Sara alikuwa na umri wa miaka tisini. Sasa angalia! Kufa kwa tumbo la uzazi la Sara ama kufa kwa mwili wake yeye hata hakukuingia mawazoni.

223 Sikilizeni haya.

> *Kwa maana ahadi ile ya kwamba atakuwa mrithi wa ulimwengu alipewa Ibrahimu na uzao wake, si kwa sheria bali kwa haki aliyohesabiwa kwa imani.*
>
> *Maana ikiwa wale wa sheria. . .wale wa sheria ndio warithi, imani* imeninii. . .*imekuwa bure, na ahadi imebatilika:*
>
> *Kwa sababu sheria ndiyo ifanyayo hasira; maana* mahali *pasipokuwapo sheria, hapana kosa.*

224 Sikilizeni hili, sasa.

> *Naye aliamini yasiyoweza kutarajiwa. . .*

“Yasiyoweza kutarajiwa,” matumaini yote yalikuwa yamekwisha! Loo, kila wakati kidogo ninapoanza kujisikia “kuhuzunika” kidogo, huu ndio mlango ninaofungua, Warumi 4, unaona.

> *(Kama ilivyoandikwa, Nimekuweka kuwa baba wa mataifa. . .); mbele zake yeye aliyemwamini, yaani Mungu, mwenye kuwahuisha wafu,* aliyeita *yale yasiyokuwako kana kwamba yamekuwako.* (“Mungu alisema hivyo!” Unaona?)
>
> *Naye aliamini kwa kutarajia yasiyoweza kutarajiwa, ili apate kuwa baba wa mataifa. . ., kama ilivyonenwa, Ndivyo utakavyokuwa uzao wako.*

225 Sasa sikilizeni, aya ya 19:

> *Yeye asiyekuwa dhaifu wa imani, hakufikiri hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa, akiwa amekwisha kupata umri wa kama miaka mia, wala hali ya kufa ya tumbo lake Sara:*
>
> *Lakini akiiona ahadi ya Mungu hakusita kwa kutokuamini, bali alitiwa nguvu kwa imani,. . . akimtukuza Mungu;*

226 Kwenye umri wa miaka mia moja? Angalia, mwili wake sasa ukiisha kufa (uanaume wake), na tumbo la Sara limekufa. Yeye ni ninii. . .Hata hilo halikufikiriwa, wakati ilipofunuliwa kwake. Kitanda hicho hakifikiriwi. Wewe umelemaa, ama chochote kile ulicho, hilo halifikiriwi. Kiti cha magurudumu

hakifikiriwi, kwa ajili ya huyo mvulana mdogo. Huenda ikawa amepooza, chochote kile alicho (sijui), hilo halifikiriwi. Hata usiliwazie.

227 "Lakini daktari alisema, 'Hatakuja hapa kamwe.' Daktari alisema, 'Hatakuja kamwe.'" Hilo hata halifikiriwi.

228 "Vema, angalia, mimi ni mzee, ninafikia kwenye umri wa makamu." Hata sifikiriwi.

229 Na sisi tu watoto wa Ibrahimu (Haleluya!), si kama alivyokuwa Isaka, lakini Mzao wake wa Kifalme (kupitia kwa Yesu Kristo) kwa imani aliyokuwa nayo, Uzao wa Ibrahimu ukitokea katika siku za mwisho kung'aa kama nyota. Watoto wa Ibrahimu! "Hakufikiria hali ya mwili wake uliokuwa umekwisha kufa." Wala hata hakuufikiria! Hata halikutiliwa shaka iwapo Mungu atafanya hivyo ama hatafanya, Mungu alisema atafanya hivyo! Kwa nini? Ilifunuliwa kwake. Hiyo ni kweli?

230 Wakati inapofunuliwa kwako, wakati kweli. . .jambo fulani. . .Huwezi kulifanya litimie, halina budi kufunuliwa kwako. Ndipo hata hufikirii jambo lingine lolote: jinsi isivyowezekana, hufikirii yale daktari aliyosema, hufikirii yale mama aliyosema, yale baba aliyosema, yale mhubiri alivyosema, yale mtu mwingine yeyote aliyosema. Unafikiria tu yale Mungu aliyosema!

231 "Hakufikiria hali ya mwili wake uliokuwa sasa umekwisha kufa, wala hali ya kufa ya tumbo lake Sara." Hata halikufikiriwa. Loo, jamani, hilo linanitikisa tu. Mwili uliokufa, wala hali ya kufa ya Sara, tumbo lake, hata havikufikiriwa.

232 Hakuna hali zitakazofikiriwa wakati imani inapopata ardhi ya kuzalia! Wakati jeni zazi kutoka kwa mwanamume inapopata ya—yai katika mwanamke, na wote wawili wana uwezo wa kuzaa, jambo fulani litatukia. Haleluya! Daktari anaweza kusema, "Hutazaa mtoto. Ninaweza kuthibitisha ya kwamba jeni za—zako zimekufa mwilini mwako, na mayai yake kamwe hayatarutubika." Lakini hebu hilo yai lililorutubika, hebu ngoja seli zazi hiyo ijinyongenyonge kwenda kwenye yai hilo wakati mmoja, angalia litakalotukia; mvulana huyo mdogo ama msichana huyo mdogo anajitokeza jukwaani. Kwa nini? Imani imepata ardhi yake ya kuzalia. Matendo yanaingia kazini, seli juu ya seli, na huyu hapa huyo jamaa mdogo anakuja. Amina. Mungu, uturehemu. Ee Mungu, laiti tungalikuwa Wakristo hodari kama ambavyo tungepaswa kuwa! Laiti tungalikuwa wanaume na wanawake ambao wangeweza kuliamini Neno la Mungu. Huwezi kufanya hivyo mpaka litakapofunuliwa kwako.

Sina budi kuharakisha.

233 Angalia, imani takatifu ya Mungu iliunganishwa na matendo matakatifu ya nabii Wake. Kumbuka, imani takatifu ya Mungu ilifunuliwa kwa Ibrahimu. Yeye aliipokea, na kwa njia hiyo

akaanza na matendo yake matakatifu, kwa kuamini. Ile mbegu ya ahadi ilikuwa na mahali pa kukulia. Vipi kama alisema (Ibrahimu) “Vema, unajua, Sara, hata hivyo, imekuwa ni miaka ishirini na mitano tangu Mungu alipofanya ahadi hiyo”? A-ha! “Kama jambo fulani lingetukia,” unaona. Lakini halingetukia. Mungu alijua halingetukia.

234 Vipi kama bikira Mariamu angalisema, “Vema, sasa, ngoja kidogo! Ati—ati bikira azae? Vema, watanifukuza kanisani mwangu kama nikiingia na kusema kitu kama hicho”? Sasa, yeye angaliwazia mawazo hayo kama isingalikuwa ni kwa ajili ya tuta hilo lililokuwa limeandaliwa.

235 Wakati nabii huyo aliposema, “Bikira atachukua mimba,” hilo lilikwisha. Unaona?

236 “Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio.” Kama tuta lipo hapo wakati Neno hilo linapoangukia pale, litashika. Hakuna kitu kinachoweza kulizuia.

237 Sasa, upesi, tunapomalizia. Unaona, ile Mbegu ilikuwa na mahali pa kujificha. Mungu alijua jambo hilo, la sivyo asingalimpa Ibrahimu ahadi hiyo. Sasa sikilizeni, kwa makini sana sasa. Mungu alijua mahali ahadi hiyo ilipokuwa inaelekea; hata hakumwita Ibrahimu mpaka alipokuwa na umri wa miaka sabini na mitano, lakini yeye alikuwa mtumishi Wake aliyechaguliwa tangu mwanzo, na Sara vivyo hivyo.

238 Angalia, kumbuka, hakuwa na Biblia ya kusoma. Mambo hayakuwa rahisi kwake kama yalivyo kwetu leo, kusoma Neno Lake na kuona wale wengine waliolikubali. Kumbukeni, yeye alilipata tu kwa ufunuo, na hilo ndilo jambo halisi. Ni vile vile kama ilivyokuwa kwa Yusufu, katika Mwanzo, hapakuwa na Biblia. Kumbukeni, Musa aliandika Mwanzo, Kutoka, Mambo ya Walawi, na Kumbukumbu la Torati. Hakuna hata mmojawapo wa hao watu pale aliyekuwa na Biblia yoyote ya kusoma mpaka baada ya Musa. Hiyo ni kweli? Hawakuwa na Biblia tuliyo nayo, ya kutusaidia katika hali yetu ya ulemavu. Walikuwa watu wajasiri ambao . . . ilifunuliwa kwao na Mungu, nao wakasimama papo hapo. Hakuna kitu kilichowatikisa. Sasa, unafikiri kwamba tungali tunaweza kuwa na imani hiyo jasiri? Kama ikifunuliwa kwako!

239 Samahani kwa tamshi hili, ama ushuhuda wakati huu, kabla tu ya kufunga. Ninakumbuka ya kwamba hapa kwenye “Twin City,” nafikiri Ndugu Brown na hao wengine walikuwa pamoja nami; nami nilikuwa nikizungumza juu ya maisha ya Yusufu, katika Biblia. Nami nikaisoma Biblia hiyo, kulikuwa na mtu mmoja humo ambaye hana lawama yoyote! Ibrahimu, Isaka, Yakobo na hao wengine wote, walikuwa na lawama, lakini si Yusufu. Ni mtu wa jinsi gani, mtu mkamilifu, mfano mkamilifu wa Kristo!

240 Niliposoma hayo, nilianza tu kulia, siku moja, katika chumba changu kidogo cha hoteli. Nami nikaingia kwenye chumba cha ndani mahali nilipotundika nguo zangu, nikafunga mlango, na nikasema, "Mungu, ninataka kukushukuru kwa ajili ya mtu kama Yusufu, mtu ambaye siku moja aliishi duniani, m—mtu mwenye mwili kama nilivyo mimi, mtu ambaye angeweza kukuamini Wewe na kulichukua Neno Lako." Alichukiwa na ndugu zake. Hangeweza kujizuia kuwa wa kiroho. Aliona ono. Aliweza kufasiri ndoto. Wote walimchukia kwa ajili ya jambo hilo. Hangeweza kujizuia kwa jambo hilo, hivyo ndivyo tu alivyokuwa.

241 Unaona, wengine hawakuwa hivyo. Walipaswa kumpenda, lakini badala ya kufanya hivyo . . . Wakati alipowaambia, wakati mwingine mambo dhidi yao, "Loo," wao wanasema, "huyu hapa yule mwotaji anakuja." Unaona? Nao wakamchukia bila sababu.

242 Nikasema, "Kwa nini wakafanya jambo hilo?" Na hata hivyo mtu huyo hakusogea, alisimama papo hapo. Unaona? Nikasema, "Asante, Bwana. Ee Mungu, nakushukuru kwa ajili ya mtu kama huyo."

243 Na papo hapo Roho Mtakatifu akanifunulia, kasema, "Utampata mtoto mwanamume, nawe utamwita jina lake 'Joseph.'" Niliamka kutoka hapo na kumshukuru Bwana.

244 Becky, anayeketi pale nyuma, alikuwa ndio tu azaliwe yapata ninii. . . . alikuwa na umri wa mwaka mmoja hivi. Alizaliwa kwa kupasuliwa, familia ya mke wangu kawaida yao ni kupasuliwa; kwa maana hawafunguki kama impasavyo mwanamke, mifupa yao ni migumu kama ya mwanamume, naye ilibidi atolewe kwa mama kwa kupasuliwa. Ndipo daktari akaniambia, akasema, "Ndugu Branham, kamwe usizae mtoto mwingine na mwanamke huyu." Kasema, "Tumbo lake la uzazi ni jembamba kama puto." Akasema, "Afadhali uniruhusu nifunge mirija hiyo."

245 Nikasema, "La, nisingeweza . . . usiwazie juu ya kulifanya jambo hilo, 'Dakt.'"

246 Akasema, "Vema, u—u—utaninii . . . Hapaswi kuzaa mtoto mwingine." Kasema, "Utamwangamiza," kasema, "atakufa." Kasema, "Hapo tulikuwa na wakati mgumu sana kule," kasema, "hebu uninii tu . . . aliponea chupuchupu."

247 Ndipo basi Bwana akaniambia nitapata "mtoto mwanamume" na jina lake litaitwa "Joseph." Sikuhofu jambo hilo kamwe. Ninyi nyote, wengi wenu, mnakumbuka.

248 Nilienda kila mahali, nikitangaza, "Nitapata mtoto; jina lake litakuwa Joseph." Ni wangapi wanakumbuka jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hakika! Kila mahali, kote nchini, kila mahali, nikiwaambia watu; "Nitapata mtoto; jina lake litakuwa Joseph."

249 Ni kama vile tu yule mtoto mdogo alivyofufuliwa, huko Finland, kutoka kwa wafu. Ndugu Jack alikuwa pale pale wakati hilo lilipotukia. Niliwaambia, miaka miwili ama mitatu kabla halijatukia, "Kutakuwa na mvulana mdogo," jinsi atakavyokuwa amevalia, mahali atakapokuwa amelala. "Mungu alisema hivyo!"

250 "Litakuwaje?"

251 "Sijui! Lakini ilifunuliwa kwangu ya kwamba lingetendeka!"

252 Ilifunuliwa kwangu, "Nilikuwa naenda Arizona, na huko ningekutana na Malaika Saba. Nao wangeniambia, na Ujumbe nitakaohubiri." Na huo ulikuwa ni ile Mihuri Saba. Ilitukia! Ni wangapi wanakumbuka nikisema jambo hilo? Kanda na kadhalika zitazungumzia jambo hilo. Na lilitimia! Magazeti, chochote kile, yaliipiga picha. Hiyo Nuru huko hewani, hata hawawezi kuifahamu hata sasa. Hiyo hapo.

253 Ninakumbuka nikimwita Ndugu Jack na kumwuliza juu ya jambo hilo, Kristo atakuwa amesimama pale, naye Ndugu Jack akasema, "Hilo ni katika umbo Lake la utukufu." Unaona? Ninampenda Ndugu Jack. Ni mmoja wa wanatheolojia hodari sana niwajuao, lakini nisingeweza tu kukubaliana nalo kabisa.

254 Nilikuwa nimesimama pale, nikasema, "Bwana, ni vipi hili? Huyu hapa ni kijana mwanamume," nikasema, "mwenye nywele kama sufu."

255 Naye akasema, "Yeye ana wigi." Angalia katika kitabu, kabla halijatukia kamwe, nilisema hivyo. Na siku hiyo wakati jambo hilo lilipotukia, lilipaa juu. Na ndipo ukiigeuza hiyo picha upande, kama una Gazeti la *Look* ama Gazeti la *Life*, igeuze upande. Huyo hapo, barabara kabisa, *Kichwa cha Kristo* aliyechorwa na Hoffman, akiangalia moja kwa moja chini mahali nilipokuwa nimesimama; Hiyo hapo gazetini! Ni wangapi waliopata kuiona? Bila shaka, nyote mmeiona. Hapo, akiangalia moja kwa moja nyuma, inathibitisha kabisa ya kwamba huo ufunuo ulikuwa ni wa kweli.

256 Ni kwa nini ana wigi? Mbona, mahakimu wa kale wa Kiingereza, mahakimu wa Kiyahudi, walikuwa wakivaa wi—wi—wigi, wangali wanafanya hivyo huko Uingereza; wakati yeye...hiyo ni mamlaka kuu, yeye huvaa wigi. Na hiyo ilimwonyesha Yeye amesimama pale, ametiwa wigi na mabawa ya Malaika, Yeye ni Alfa na Omega. Yeye ni Hakimu Mkuu, wala hakuna mwingine ila Yeye. Yeye anaonekana mithili ya Alfa na Omega. Naye huyo hapo kijana mwanamume, hajapita umri wa miaka thelathini, amevaa wigi nyeupe. Ikionyesha ya kwamba Yeye alikuwa ni Mwenyezi, Mungu, "Baba ameweka hukumu *yote* mikononi mwa Mwana." Haleluya! Huo ufunuo haukosei kamwe! Nena habari Zake hata hivyo, hata usikike namna gani, unaambatana moja kwa moja na Neno.

Sasa kukumbuka, miaka minne baadaye, mke wangu . . .

257 Tulijua tutapata mtoto. Kila mtu alisema, “Je! huyu anayekuja ni Joseph?”

258 Nikasema, “Nadhani ndiye, sijui, lakini nitampata Joseph.”

259 Mtoto alipozaliwa, alikuwa ni Sara. Ndipo mtu fulani akanipigia simu, akanidhihaki papo hapo, akasema, “Ati, wajua nini? Ulimaanisha Josphine!” (Mtu huyo alikufa. Mtu huyo alikufa.)

260 Nikasema, “Bwana, nikasema, ‘Mungu aliniambia nitapata “mwana” nami “nitamwita jina lake ‘Joseph’”!’”

261 Kulitokea watu watatu walioacha kanisa fulani la kimadhehebu wakaja kwenye kanisa letu, nao wakanisikia nikisema hivyo. Wakati Sara alipozaliwa, wakasema, “Mbona, yeye ni nabii wa uongo.”

262 Nikasema, “Ngojeni kidogo, enyi mabibi, sikusema kamwe kwamba ni *lini*, wala Mungu hakusema ni *lini*. Yeye aliniambia, ‘utapata m- . . .’ Ataninii . . . alimwambia Ibrahimu, ninyi ‘mtampata Isaka,’ lakini Ishmaeli alizaliwa katikati ya wakati huo, bali hilo halikulibatilisha.” Nikasema, “Mungu alisema nitampata mvulana huyu naye atamwita jina lake ‘Joseph.’”

263 Daktari akasema, mtoto alipokuja, akasema, “Kasisi, nitafunga mirija hiyo sasa.” Nikasema, “Mimi . . . ”

264 Nikasema, “Usifanye hivyo!” Nikasema . . .

265 Akasema, “Vema, huenda ukaoa tena na ukampata mvulana huyo bado.”

266 Nikasema, “Nitampata kwake! Mungu alisema hivyo!” Singeweza kusoma hilo katika Biblia lakini lilikuwa limeandikwa moyoni mwangu kwa ufunuo, kwa imani; Mungu alisema hivyo! Sikutaka kusitasita katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini.

Baadhi yao walisema, “Ulimaanisha ‘Josephine.’”

Nikasema, “Nilimaanisha ‘Joseph.’”

Daktari alisema, “Hawezi kuzaa mtoto mwingine.”

Nikasema, “Atazaa mtoto mwingine.”

267 Miaka minne ikapita, hatimaye akawa mja mzito tena.

268 Halafu mwanamke fulani, (unabii wa uongo ulioenezwa kote nchini) aliandika maneno, akasema, “Sasa, Meda atakufa, kipindi hiki, kwa maana nilitumwa kumwongoza Bill.” Na ukasema ya kwamba “Yeye hatanisikiliza ati kwa sababu mimi ni mwanamke, na Mungu atampatiliza sasa kwa kumwua mkewe.”

269 Nikasema, “Mungu alimtuma Yesu Kristo kuniongoza.” Unaona? Nami nikasema, “Mimi ninaongozwa na Roho.”

270 Maskini Meda. Tulikuwa na nesi aliyekuwa ameponywa kule kwenye mikutano, nyote mnamjua, Bibi Morgan, (na ni mmoja wa manesi wa Mayo, akiwa mahututi sana). Vema, yeye yuko kwenye kumbukumbu kwamba, "ameshakufa," kama miaka ishirini iliyopita, kwa "kansa, kansa ya sarkoma," huko Louisville, papo hapo kwenye kumbukumbu za hospitali ya Kibaptisti. Yeye anafanya ukunga huko—huko Jeffersonville, hospitalini, sasa. Amekuwa huko kwa miaka hii yote, maana Mungu alisema "Ataishi."

271 Na, kwa hiyo, Meda alimpenda, basi akasema, "Ninataka Margie aambatane nami, Bill, sijisikii kwenda hospitalini."

272 Nikasema, "Usifanye ninii . . . Tunampenda Margie, lakini Margie siye Mungu wetu, Margie ni dada yetu." Nami nikaenda moja kwa moja huko Green's Mill. Amenitibua sana. Bila shaka, ninampenda. Nikaenda huko Green's Mill.

273 Naye akasema, "Bill, unafikiri nitakufa?"

274 Nami nikasema, "Sijui, lakini huyo mtoto atazaliwa, hata hivyo. Utamzaa Joseph."

275 Akasema, "Ni huyu?"

276 Nikasema, "Sijui, Mpenzi. Siwezi kusema, lakini Mungu alisema 'atamzaa Joseph,' nasi tutampata Joseph. Sijali chochote kinasema nini, tutampata Joseph. Kwa maana, Mungu yeye yule ambaye ameniambia funuo hizi zote, aliniambia jambo *hilo,* Yeye hakushindwa katika hayo mengine wala hatashindwa katika huo."

277 Nikapanda, kwenda kwenye huo mtambo, kuomba. Ndipo nikaanza kuelekea huko. Hiyo hapo ile Nuru imening'inia katikati ya miti miwili, kasema, "Rudi kwenye Neno lako, kwenye kile kitabu."

278 Nikarudi kwenye Biblia, nayo ilikuwa kwenye gari langu. Na nilipofanya hivyo, upepo ulikuwa umeifunua mahali pale ambapo Nathani alikuwa ameketi, na Daudi; alisema, "Nenda ukamwambie mtumishi Wangu Daudi; nilimtoa katika hilo zizi la kondoo, toka katika kuwalisha hao kondoo wachache wa baba yake, nami nikamfanyia jina kuu kama mtu mkuu." (si ninii yote—jina lililo kuu kuliko yote, lakini *kama* tu mtu mkuu; kamwe sikumfanya Billy Graham, lakini ninii . . . nilimpa jina, unajua) Kasema, "Nimefanya jambo hilo, lakini" kasema, "siwezi kumwacha anijengee hekalu, lakini mwanawe . . . " Na mara tu iliposema, "Wanawe," loo, jamani, hilo hapo.

279 Nikasema, "Joseph?" Hiyo ni kweli.

280 Nikaenda nyumbani moja kwa moja. Na huyo hapo maskini jamaa huyo, mkubwa sana, mama, maskini mvulana mkubwa, ilikuwa ni vigumu kwake kutembea, akapitia uwanjani. Nikakimbia, nikamkumbatia, na kusema, "Mpenzi! Joseph yuaja. Joseph yuko njiani."

281 Kila mtu anajua, kwa wanaopasuliwa, huwezi kumwacha mtoto mchanga adondoke. Usiku huo mtoto alidondoka, maji yakavuja, mengine yote.

282 Kesho yake asubuhi, saa moja, tukaenda hospitalini, daktari akasema, "Loo, salalaa, jamani."

283 Nikambusu kwa heri, nikasema "Mpenzi, haitachukua muda mrefu, Joseph atakuwa hapa." Moja kwa moja akapanda vipandio, namna hiyo, kwenye meza ya upasuaji.

284 Mnamo dakika chache, nesi akashuka akaja, kasema, "Kasisi Branham?"

285 Nikasema, "Naam, mama."

286 Akasema, "Umepata mvulana mzuri, mwenye ratili saba, wakia tatu."

287 Nikasema, "Joseph, mwanangu, karibu." Naam, bwana! Kwa nini? Kwa nini? Ni kitu gani? Haikuandikwa katika Biblia kwamba hilo lingetukia, lakini Mungu yeye yule wa Biblia aliyemfunulia Ibrahimu jambo hilo, hatukufikiria hali ya kufa kwa tumbo lake, kutokuwezekana kwake. Husitasiti katika ahadi ya Mungu kwa kutokuamini, lakini unampa Mungu sifa, unajua ya kwamba halina budi kutukia! Sijali daktari anasema nini, kila kitu kinginecho kitakuja kwa njia ya kila namna, lakini usiamini jambo hilo, ni uongo wa Ibilisi. Naam, bwana, kweli. Imani inaenda kila mahali, pamoja na matendo, kuumba hiyo ahadi. (Hebu tuharakishe)

288 Ni sawasawa kabisa na vile ilivyosema, "Kahaba Rahabu," Yakobo alisema, "alihesabiwa haki kwa matendo." Lakini ni kwa nini? Imani yake!

289 Alisema, "Ninasikia ya kwamba Mungu yu pamoja nanyi." Hakutaka kuona jinsi Yoshua alivyochana nywele zake, ama jinsi alivyovaa nguo zake. Alisema, "Ninasikia ya kwamba Mungu yu pamoja nanyi." Hilo ndilo tu lililokuwa linahitajika, akajitayarisha.

290 Kama vile tu ono la kweli leo, (ninafunga tu sasa hivi) maono ya kweli kutoka kwa Mungu leo, ni Neno lililoahidiwa kwa ajili ya siku hii. Unasema, "Maono haya, Ndugu Branham, unayapata hayo wapi?" Watu wanajikwaa kwenye jambo hilo. Je! hivi Matendo 2:17, haikusema, "Itakuwa katika siku za mwisho ya kwamba vijana wenu wanaume wataona maono, wazee wenu wataota ndoto"? Hiyo si ni kweli? Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema.

291 Vema, sasa kama jambo hilo ni kweli, pia angalia Malaki, mlango wa 4, na uone kama hili halijaahidiwa leo. Unawezaje kuwa na imani katika jambo Hilo? Biblia ilisema hivyo!

292 Sasa chukua Luka 17:30 na uisome. Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja Kwake Mwana wa Adamu." Kama tu ilivyokuwa Sodoma.

Sasa, angalia hali ya ulimwengu siku hizi: Walawiti. Mwangalie yule Billy Graham na Oral Roberts, hao mashahidi wawili, chini kule wakishuhudia makanisa ya kimadhehebu. Mmoja kwa Wamethodisti, Wabaptisti, na Wapresbiteri; huyo mwingine kwa Wapentekoste. *Huyu, yule* na *yule mwingine*.

293 Lakini kumbukeni, Ibrahimu hakuwa Sodoma, alikuwa tayari ameitwa atoke. Na kuna Mmoja aliyebaki na kuzungumza naye! Na Yule aliyebaki na kuzungumza naye, alimwonyesha *yeye* ishara. Akiwa amempa kisogo, alisema Sara atampata mtoto ambaye alikuwa amemngojea. Amina. Akiwa amempa kisogo. Naye akamwita Huyo, "Mungu, Elohimu."

294 Sasa, hilo linatimia leo, kwa sababu tuna imani. Nami ninajua hili ni la Mungu, ni kwa sababu hili na Maandiko mengine yanaelekeza kwenye saa hii. Ufunuo 10, ilisema ya kwamba "katika wakati wa Ujumbe wa malaika wa saba, atakapoanza kutangaza Ujumbe wake," si katika ibada za kuponya, lakini ni ule Ujumbe unaofuata ibada ya uponyaji.

295 Yesu alitoka akaenda kuhubiri. Alisema, "Aliwaponya wagonjwa, na kila kitu. Loo, huyo Rabi kijana, nabii huyo, Yeye ni mtu mashuhuri. Tunamtaka kanisani mwetu."

296 Lakini siku moja Yeye alisimama, kasema, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja." Loo, jamani. Hawakumtaka tena. Naam. Loo!

297 "Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa damu Yake!" Yeye hakuelezea jambo Hilo. Kasema, "Msipoula mwili wa Mwana wa Adamu, na kuinywa damu Yake, hamna Uzima ndani yenu."

298 Mbona, nawazia, baadhi ya madaktari na manesi walisema, "Mtu huyu ni kizuu kifyonza damu, anajaribu kutufanya tunywe damu yake." Unaona, hawakufahamu jambo Hilo. Yeye alijua hayo.

299 Lakini hao wanafunzi, huenda hawangeweza kueleza jambo hilo, lakini waliketi pale na kuliamini hata hivyo, amina, kwa maana lilifunuliwa kwao. Naam, bwana. Walijua jambo Hilo, Maandiko yalikuwa yamelitangaza.

300 Ningeweza kuulizwa basi hili, kama mngesema, "Kwa nini una imani ya kuamini maono haya, wakati—wakati kuna kuiga kwingi sana kunakoendelea?"

301 Nitazungumzia jambo fulani dogo, kali, kwa muda kidogo tu sasa. Wakati kuna kuiga kwingi sana kwa uongo hapa, kumbuka, ndugu yangu, wamenenwa pia ya kwamba watakuwapo hapa wakati huu. Hiyo ni kweli kabisa, kama tu ilivyokuwa katika wakati wa Musa. Musa alishuka akaenda kufanya kazi za Mungu mbele ya watu, na kulikuwa na Yambre na Yane waliokuwa wamesimama pale. Lakini ni nani aliyekuwa wa kwanza kufanya jambo hilo? Kwa hiyo hawa wengine walikuwa ni waigaji, maana ilibidi kuwe na wa asili kwanza wao wapate kumwigiza.

Kama hao walikuwa ndio wa asili...A-ha. La, sisi hatu—sisi hatujapotea. Tunajua mahali tulipo, unaona, unaona, kwa Maandiko na kwa ufunuo wa Mungu. Hiyo ndiyo sababu ungali unasimama.

302 "Mbona, mtu *huyu*, yeye anaona maono na kadhalika. Anafanya *hivi*, na anazurura na mke wa mtu *huyu*. Yeye anaamini katika—katika miungu watatu, na mambo haya yote." Hilo haliyumbishi hata kidogo. Na hiki hapa kitu kimoja wasichoweza kuigiza: lile Neno! Angalia. Wanaweza kuwa na mambo yote haya, wanaweza kunena kwa lugha, wanaweza kupiga makelele, kucheza katika Roho, na bado wawe ni pepo. A-ha. Hiyo ni kweli. Hiyo ni kweli. Lakini Neno hili huwapima. Unaona? Hiyo ni kweli kabisa. Hapa ndipo linapofikia. Kama vile Musa, na Yambre...

Basi kumbukeni, Yeye alisema, "Kama vile Yambre na Yane walivyompinga Musa, katika siku za mwisho hawa waigaji hawa watainuka katika nchi tena." Je! Yeye alisema jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Vema, tunao.

303 Lakini hilo halikumyumbisha Musa. Wakati Musa alipogeuka na kutenda muujiza katika Jina la Bwana, na hapa walisimama hawa waigaji, wakafanya jambo lile lile. Hilo halikumzuia, aseme, "Vema, afadhali niache na niondoke kwenye huduma." Alikaa papo hapo. Kwa sababu gani? Ilifunuliwa kwake. Haleluya! Yeye alijua kwa Neno la Mungu. Alijua ya kwamba Neno hatimaye lingewafichua. Alijua ungekuja wakati Neno lingejidhihirisha Lenyewe, nao wasingeweza kuendelea mbele zaidi.

304 Vivyo hivyo nimejua jambo hili, miaka hii yote, unaona, hiyo ni kweli, ya kwamba wakati huo ungekuja. Wakati mwujiza wote ambao Mungu anatuma, mwujiza halisi, daima kuna badiliko katika mfumo huo wote. Kama Mungu akituma kitu fulani kanisani, na ule mfumo wa kale haujabadilishwa, Yeye alituma kitu hicho bure. Wakati ujumbe unapotangazwa kwa ishara na maajabu, kuna Ujumbe unaoufuata. Wakati Yesu alipotoka akaenda akiwaponya wagonjwa, ndipo Ujumbe Wake ulikuja, "Mimi na Baba Yangu ni Mmoja. Mimi Ndiye." Unaona? Unaona, wao—wao hawakuamini jambo Hilo. Waliamini miujiza Yake. Kasema, "Kama hamwezi kuniamini Mimi, aminini hiyo miujiza, kwa maana inawashuhudia, Mimi ni nani." Loo, jamani. Utukufu! Ni nani aliyekuwa wa kwanza? Musa! Ndipo wakamwigiza. Lakini zile kweli kuu zinabakia vile vile kati ya kweli na uongo, wao hawawezi kuukubali Ujumbe! Hawawezi kukubali Ujumbe ambao haujaghoshiwa, kutoka kwenye Neno la Mungu.

305 Sijali, Yuda angaliweza kufanya kila namna ya ishara na maajabu; lakini, ilipofikia kumpokea Roho Mtakatifu kwenye Siku ya Pentekoste, alionyesha rangi zake. Huyo ibilisi

anaweza kuja moja kwa moja na kuiga kufikia kwenye kitu chenyewe kabisa, mpaka inafikia kwenye Neno hili, bali hawezi kuchukua hilo Neno lote. Anaweza kulileta lote, labda mpaka kwenye kubakiza Neno moja kama vile Hawa alivyofanya, Ibilisi alivyomfanyia Hawa, lakini hawezi kulivuka lote. Kwa sababu ninii pekee...kitu chote kizima ni Mwili wa Kristo. Unaona, Neno sasa. Wala hawangeninii...Hawangeweza, hawawezi kuchukua Ujumbe sasa, wala akina Yambre na Yane hawangeweza kuchukua Ujumbe wa Musa. Hawangeweza kuuchukua. Kazi zao za kuigiza zilifichuliwa, kwa maana hawakuweza kufuata Neno la Mungu lililothibitishwa na nabii Wake aliyetiwa mafuta. Unaona?

306 Hawangeweza kuwafuata Israeli watoke pamoja nao. Kwa nini? Walikuwa watoto wachanga wa madhehebu ya Kimisri! Hawangeweza kulifuata Neno hilo. Kama wangelilifuata, ingewabidi kuondoka Misri. Naili, mambo yote yalikuwa mazuri kwao, nao hawangeweza kuondoka. Ingawa wangeweza kuiga zile kazi, na kufanya yale Musa aliyofanya, lakini upumbavu wao ulifanywa dhahiri ilipofikia wakati wa kuondoka. Ndipo Mungu kweli akaimiminia kweli kweli, juu yao.

307 Ndivyo ilivyo sasa! Wanaweza kufanya kila namna ya maigizo ya uongo na kadhalika, hilo halifanyi kitu ila kulikuza tu jambo lililo la kweli. Na mtoto yeyote anayeamini anajua jambo hilo ni Kweli. A-ha. Hapa unaona dhahiri, basi, kazi za upumbavu wao wa kuigiza kwao. Kama ninii yako—kama kazi zako ni Neno la kweli na zinathibitishwa Nalo, kwa imani yako, zitadhihirika na kama ahadi ya Mungu, katika Neno Lake la asili lililoandikwa.

308 Yesu alisema, "Kama nisipozitenda kazi..." Sikilizeni kwa makini! "Kama nisipozitenda kazi..." Hebu niongeze jambo hili Kwake. "Hiyo ni kusema, kama sizitendi kazi ambazo Maandiko yanawaambia nitazitenda, basi...kuzifanya hizo katika wakati Wangu, nitakapokuja, kile Masihi alichopaswa kufanya atakapokuja. Kama mambo nifanyayo, kama Mungu hathibitishi Neno hilo ambalo alisema lingetimia, kama maisha Yangu hayalifanyi Neno hilo kuwa hai vile vile hasa lilivyosema lingefanya..." Msikose jambo hili! Yesu akisema, "Mnajua yale Masihi anayopaswa kufanya. Basi, kama Neno hilo lililoandikwa, na halafu halijidhihirishi Lenyewe kupitia kwangu Mimi, basi Mimi siye." Amina! "Basi ile siku ninayonena habari zake siyo, yale Yohana aliyosema juu yangu hayakuwa ya kweli. Halafu basi iwapo Mimi siye huyo Masihi, kama kazi hizo ambazo Masihi alipaswa kufanya. Yeye atakuwa 'Bwana Mungu wenu atawaondokeshea nabii mithili yangu,' nanyi hamjawa na nabii kwa mamia ya miaka. Na kama hizo kazi nizifanyazo Mimi, ambazo Mungu aliahidi, kama hazidhihirishwi katika maisha Yangu ya sasa hivi, basi Mimi siye. Lakini kama Neno lililoahidiwa la wakati huu linathibitishwa ndani Yangu, basi

Mimi Ndiye na ile ahadi imewajilia." Loo, jamani, sioni jinsi gani lingeweza kuwa dhahiri zaidi! "Kama ile ahadi haininii . . ." Loo!

309 "Basi kama ahadi ya siku hiyo imedhihirishwa katika huduma Yangu," Yesu alisema, "basi Mimi Ndiye. Basi kama ni vigumu kwenu kuamini kwamba Mimi ni nani, basi angalieni zile kazi zilizoahidiwa kwa ajili ya siku hii." Amina! "Angalieni zile kazi zilizoahidiwa. Kama kazi hizo hazitimizwi, kila moja ya kazi hizo ndani Yangu, basi msiniamini Mimi, kwa maana nimewadanganya. Hamwezi kuniamini Mimi, hebu angalieni tu yale Biblia ilisema yangetukia katika siku hii. Kama hayatendeki, basi ni uongo. Kama mambo haya ya uongo hayapo hapa, na mambo haya mengine yote, na mambo yanayopaswa kutukia; kama hayapo hapa, basi nimekosea. Lakini kama yapo," Yesu alisema, "basi Mimi Ndiye." Amina! "Mimi Ndiye niliyeahidiwa kuja."

Loo, jamani, kazi zile zile zilizoahidiwa, katika siku Zake, zilimthibitisha *Yeye* kuwa ndiye Masihi huyo. Je! hamwamini jambo hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

310 Vema, sasa, ndugu, kama kazi za Luka, mlango wa 17 na kifungu cha 30, ile ahadi ya Yesu Kristo, kabla tu ya kuja Kwake, ya kwamba ulimwengu ungerudia kuwa Sodoma na hao wajumbe wangetoka, na mambo hayo yatafanywa jinsi ile ile hasa; kama jambo hilo halitukii, basi msiniamini kwamba nimewaambia Kweli. Bali kama yanatukia, basi aminini kwamba ni Yeye, "Katika siku ile Mwana wa Adamu atakapofunuliwa." Amina! Mwana wa Adamu atafunuliwa katika mwili wa nyama, enyi watu Kanisa, kabisa kama tu vile ilivyokuwa kabla ya siku za Sodoma, kundi lililoitwa litoke kutoka kwa hao wote, wametoka, wakiamini ahadi ya Mungu. Utukufu!

311 Basi, kazi ambazo Roho Mtakatifu anazifanya siku hizi, kwa maono haya yasiyoshindwa, ahadi zisizoshindwa, ishara zote za kimitume zilizoahidiwa katika Biblia, za Malaki 4, na, loo, Ufunuo 10:7, yote hayo yanatimia; na kuthibitishwa kisayansi, kwa njia yoyote ile. Na kama sijawaambia Kweli, mambo haya hayangetendeka. Lakini kama nimewaambia Kweli, yanashuhudia ya kwamba nimewaambia Kweli. Angali ni yeye yule jana, leo, na hata milele, na madhihirisho ya Roho Wake yanamnyakua Bibi-arusi. Hebu imani hiyo (ufunuo) iangukie ndani ya moyo wako, ya kwamba "*Hii* ndiyo ile saa."

Sasa hebu na tuombe.

312 Mungu mpendwa, uliyedhihirishwa katika mwili katika utu wa Yesu Kristo, aliyefufuka toka katika wafu, siku ya tatu, kulingana na Maandiko, na ukapaa Juu, na ukawatuma wanafunzi kuufanya ulimwengu wote kuwa wanafunzi, na kusema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

313 Mungu, kwa kanisa la Kipentekoste la siku hii, kurudishwa kwa karama; jalia, Bwana, watu hao, labda wengine wao wapo hapa, wengine wao wanasikiliza kanda kote ulimwenguni, jalia watambue ya kwamba huku ni kuitwa kwa Bibi-arusi, wala si ujumbe wa Kipentekoste. Ujumbe wa Kipentekoste ulikuwa ni wa kurudisha karama Kanisani. Lakini huku ni kuitwa kwa Bibi-arusi, Ujumbe mwingine uliokuwa uje kabla tu ya Sodoma kuteketezwa kwa moto. Jalia wafahamu, Mungu mpenzi. Imani, ninaliamini Hili, kwa sababu limefunuliwa na Roho Wako kupitia kwenye Neno la Mungu na limethibitishwa na kudhihirishwa ulimwenguni kote. Hakika, Bwana, katika uchache, daima makundi Yako yako hivyo. Lakini ulisema, "Msiogope, enyi kundi dogo, ni mapenzi ya Baba yenu kuwapa ninyi ule Ufalme."

314 Kwa hiyo, naomba, Mungu, ya kwamba mwanadamu ataacha kutegemea akili zake, ataacha kutegemea yale wanayoweza kufikiria kwamba ni ya kweli, na waangalie katika Maandiko. Na kama ilivyonenwa jana usiku, jalia watu hapa wafikirie kama yule malkia alivyofikiri katika siku za yale maangamizi makuu ya Babeli, yeye alisema, "Kuna mtu miongoni mwenu aitwaye 'Danieli,' alikuwa katika ufalme wa baba yako. Huyo baba wa kipentekoste alikuwa katika ufalme wake, Naye huondoa mashaka yote."

315 Na sasa, Bwana, jalia Roho Mtakatifu aliyekuwa katika ufalme wa kipentekoste, ufalme uliokuwa wa Martin Luther, uliokuwa wa John Wesley, na—na kuendelea mpaka kwa John Smith na Alexander Campbell, na kote kote katika wakati. Yeye ndiye Mwenye Kuondoa, aliondoa mawazo. Na ninii—na watu katika siku za Luther, mtu huyo, "Mwenye haki ataishi kwa imani." Wamethodisti, Yeye aliondoa mawazo yote, ya kwamba "Wanapaswa—wanapaswa kutakaswa." Na katika siku za pentekoste, wao walinena kwa lugha, wakatoa madhihirisho ya Roho kwa uponyaji wa Kiungu na kadhalika, Yeye aliondoa mashaka yote katika moyo wa kipentekoste. Lakini, Ee Mungu, wao waliunda madhehebu. Walirudi moja kwa moja kuchukua mawazo ya mwanadamu. Kwa hiyo, sasa wakati Bibi-arusi anapoitwa atoke kama ulivyoahidi jambo hilo hapa katika Maandiko, tukiyasoma mbele za ulimwengu, usiku baada ya usiku, nasi tunaliangalia kwa macho yetu. Mungu, naomba liondoe mashaka yote katika mioyo ya watu. Jalia wakimbie upesi waende kwa Mwana aliyefunuliwa, wapate kuivishwa, wapelekwe ghalani wala wasiachwe katika shina wakachomwe, lakini na waende ghalani usiku wa leo. Katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Nashukuru kwa utulivu wenu. Mungu na aushughulikie moyo wako.

316 Sasa, hivi wewe. . .Tuna kadi za maombi zilizosambazwa. Sasa, tutachukua kama dakika ishirini sasa, kwa ajili ya mstari

wa maombi. Tunataka kufanya mstari upesi sana, na mje jukwaani tuombe. Na sasa, sijui ni kadi ngapi zilizotolewa. Hata sikumwuliza Billy neno lolote. Nilisema tu, "Je! ulisambaza . . . Shuka uende kule ukasambaze kadi chache." Naye akarudi na kumchukua mama yake pamoja na mimi na hao wengine, muda kidogo tu uliopita. Sasa, ni—ni- . . . je! . . .

317 Vema, ulianza na mia moja, ama moja, na moja hadi mia moja, ama ipi? [Ndugu Billy Paul anasema, "Moja mpaka mia moja."—Mh.] Moja mpaka mia moja. Vema.

318 Hebu na tuchukue kadi ya maombi namba moja. Kama unayo, inua mkono wako ili niweze kuona. Kama huwezi . . . Kama unaweza kusimama . . . kama huwezi, tutakubeba. Kadi ya maombi namba moja, upesi sana. Ni nani aliye na hiyo? Unasema nini? A, namba moja. (samahani) A, namba . . . Bibi huyu hapa, je! una kadi hiyo? Njoo moja kwa moja hapa, sawa bibi? A, namba mbili. Unayo, mtu fulani? Inua mkono wako upesi. Papa hapa, bibi, njoo. Namba tatu. Una kadi? Una kadi? Ninyi nyote hamna kadi zozote, hata kadi moja? En-he? Vema, si lazima uwe nayo. Tatu, nne, tano. A, moja, mbili, tatu, nne, tano. Hebu tuone, kuna moja, mbili, tatu, nne, tano. A . . . Vema, hapa wao . . . Tano, sita, saba, nane, tisa, kumi. Vema, pangeni tu mstari, anzeni tu kufanya mstari.

319 Sasa, kama huwezi kuja, punga mkono wako namna hiyo ili waweze kukubeba. Nimewaomba watu hawa hapa, ambao hawana kadi . . . Si lazima muwe nazo, ninawauliza tu. Sasa angalieni, ninyi—ninyi watu walemavu hapa, ninadhani ilimbidi kuja mapema, maana, yeye, nilimwambia sasa hivi "mapema." Sasa, si lazima uwe na kadi, kama una imani kama hiyo nilivyoifundisha. Unaona, kama imefunuliwa kwako, vema. Kama haijafunuliwa, haidhuru kama utakuwa katika mistari ya maombi dazani moja, isingekusaidia hata kidogo. Unajua jambo hilo? Unaamini jambo hilo? Unaona? Huenda niombe, nifanye yote niwezayo, nipige magoti, na kukuwekea mikono, nikupake mafuta, vyovyote vile ulivyotaka, na kuomba. Mpaka Mungu, kwa neema, akufunulie jambo hilo moyoni mwako, ya kwamba "Imekwisha," basi imekwisha. Haikubidi hata kuwa kwenye mstari ama popote pale, imekwisha haidhuru.

320 Vema, nne . . . Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi, kumi na moja, kumi na mbili, kumi na tatu, kumi na nne, kumi na tano. Vema, kumi na sita, kumi na saba, kumi na nane, kumi na tisa, ishirini. Kuna mtu nimemwita aliye na kadi ya maombi na hawezi kuamka? Inua mkono wako, una kadi na huwezi kuamka. Vema.

> . . . amini tu,

Ninaweza kumwona maskini, binti mpendwa Anna Jeanne ameketi, akipiga huo usiku kucha, karibu usiku kucha, wakati

mwingine. Ninataka kila mtu atulie kabisa na awe na kicho hapa ndani, kama mjuavyo.

. . . aminini tu;

Sasa, kadi za maombi moja mpaka kumi na tano, ninaamini ilikuwa hivyo.

. . . amini tu,

Wanasongamana kidogo hapa, kwa hiyo hebu—hebu tuanze tu. Unasemaje?

. . . yatendeka . . .

321 Moja, mbili, tatu, nne, tano, sita, saba, nane, tisa, kumi . . . Sasa, mnakuwa wengi mno. Hao ni zaidi ya wale tuliowaita. Hilo ni sawa. Tulieni, mahali tu mlipo. Mtu yeyote asininii tu . . . mtapata . . . Mtaombewa, lakini ninii tu . . . Mnaona, ngojeni tu mpaka watakapoita namba yako. Halafu, mwajua, hatutakuwa na wengi mno waliosimama hapa. Kama Bwana akifanya jambo fulani, mtawazuia na hawawezi kuliona, mnaona. Mungu awabariki.

Sasa hebu tuombee leso hizi wakiwa wanajitayarisha.

322 Mungu mpenzi, hapa kuna leso zilizo hapa zinazotoka kwa wagonjwa na wanaoteseka. Hii imani ambayo ndiyo kwanza tuzungumze habari zake, Bwana; ninakumbuka Wewe ukisema, katika Biblia, katika Kitabu cha Yuda, "Muishindanie kwa bidii imani waliyokabidhiwa watakatifu mara moja tu." Na kutoka kwenye mwili wa watakatifu walichukua leso, si kwa sababu eti walikuwa watu maalum, lakini ni kwa sababu walikuwa watu wanaoamini. Walikuwa watu wenye tabia moja na sisi. Walisema, "Eliya" alikuwa namna hiyo naye "akaomba kwa bidii mvua isinyeshe." Na, Mungu, aliomba *hivyo* ili watu wapate kutubu. Ulimfunulia ili awaombee, kuomba kwa namna hiyo ili kutimiza Neno Lako. Hapana shaka ulimwonyesha nabii huyo ono. Na, Bwana, usiku wa leo ninawaombea watu hawa waponywe. Mimi si Eliya, yeye alichukuliwa Mbinguni, lakini Maisha yake na Roho yake ingali inaishi. Kwa hiyo tunaomba, Mungu mpendwa, ya kwamba Wewe utaheshimu maombi ya watu Wako. Na utujalie sisi sote sasa tunapoombea leso hizi, ili kwamba zitakapowekwa juu ya wagonjwa watapata afya.

323 Tunatambua, Baba, ya kwamba sisi ni kizazi cha watu wanao—wanaokufa. Tunaelekea . . . kabiliwa—kabiliwa na Umilele. Ulimwengu umeenda wazimu. Mauaji; wasichana wadogo wakikatwa vipande-vipande na kunajisiwa. Watu, wanaume wakitengeneza nywele zao kama wanawake, wanawake kama wanaume, wanapotosha tu. Jamii inakufa. Ulimwengu unakufa. Kila kitu kinakufa. Kanisa linakufa.

324 Ee Mungu, lete Uzima. Lete Uzima, Ee Mungu, Uzima wa imani. Wafunulie watu hawa, Bwana. Ninaweza tu kuomba na kuweka mikono yangu juu yao. Lakini Wewe ndiwe unayeweza

kuwaponya, na Wewe pekee ndiwe unayeweza kuwaponya. Ninaomba ya kwamba utawaponya, Baba, kila mmoja wao. Tujalie, nikiwa nimewawekea mikono yangu, na kuomba kwa moyo wangu wote; katika Jina la Yesu Kristo, waponye watu hawa. Amina.

325 Sasa, hii maiki inafanya kazi, ndugu? Sasa mnasikia hayo vizuri? Kila mtu anasikia hayo? Inua mkono wako. Vema. Sasa, kwa namna fulani, moyo wangu unawapenda watu hawa hapa, wanaoketi hapa katika ninii hii—kiti hiki, vitanda vidogo na machela . . . hao "hata hawakupata kadi ya maombi." Unaona? Lakini, angalia, ndugu, unaona, watu hawa walipata kadi za maombi, lakini hilo halimaanishi wataponywa. Kuna watu wanaoketi huko kwa wasikilizaji, labda, hilo—hilo—hilo halimaanishi wata—wata—wataponywa. Hilo—hilo halisemi ya kwamba—ya kwamba wataponywa ama hawataponywa. Hilo lote linategemea imani yao katika Mungu. Ni wangapi wanajua jambo hilo kuwa ni kweli? Hivyo tu, imani yao tu katika Mungu. Vema, sasa, ni wangapi wanajua ya kwamba hiyo ni kweli? Haidhuru wewe ni wa kidini jinsi gani, jinsi ulivyo mzuri ama mbaya, neema ya Mungu isipoidondosha hiyo moyoni mwako, hutapona kamwe. Sasa, ni wangapi wanajua ya kwamba Mungu amefanya jambo hilo, amelitenda wakati wote, miujiza mikubwa, ishara na maajabu? Na sasa, unakuja usiku wa leo, ukisimama kwenye mstari huu, si kwa sababu ulichaguliwa kusimama kwenye mstari huu na Mungu, si hivyo; ulipata tu kadi ya maombi, ilitokea tu kwamba ilikuwa kwenye ninii yako . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

326 Utaratibu ni jinsi tu vile hasa Ndugu yangu mnyofu Gerholzer hapa, alivyoanza huduma yake miaka mingi iliyopita. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . akiwa na imani katika Mungu, akimwamini Mungu, akiamini ya kwamba Mungu aliwaponya wagonjwa kwa imani. Wala haijabadilika kamwe, lakini Mungu ameongeza katika siku hii ya mwisho, karama, karama alizoahidi. Mungu alifanya jambo hilo kwa sa- . . . si sababu ilimbidi kuzileta, lakini ni kwa sababu Yeye aliahidi kuzileta. Na kama aliahidi, basi Yeye hana budi kufanya hivyo; kwa maana hana budi kutimiza Neno Lake.

327 Naye aliwaahidi ninyi jambo lile lile, yaani, "Kama ungeweza kuamini ya kwamba litatendeka." Kama huwezi kuamini Hilo, ni kwamba tu halitatendeka. Sasa, siwezi kukufanya uamini, wala huwezi kujifanya uamini. Mungu hana budi kukupa jambo hilo. Ni karama ya Mungu, kuamini. Si imani yako, imani ya Mungu. Imani yako ya kiakili inaweza kuamini vizuri kabisa, lakini isipokuwa imani ya Mungu iwe ndani ya moyo wako . . . Unaona, imani yako ya kiakili inaweza kukubali, kufanya jambo hilo. Basi endelea tu kuamini hilo kwa moyo wako wote mpaka Mungu atakapokufunulia jambo hilo.

Unaona? Endelea tu kuliamini mpaka Mungu alifunue. Lakini mpaka atakapolifunua . . .

328 Unasema, "Ndugu Branham, ungesema nini hapo?"

329 "Naam, bwana!" Mungu alimtuma nabii kwa Hezekia na kumwambia, "'Hutatoka kwenye kitanda hicho,' BWANA ASEMA HIVI. 'Utafia hapo kwenye kitanda hicho.'" Hiyo ni kweli?

330 Lakini nabii huyo aligeuka . . . ama mfalme huyo alielekeza uso wake ukutani, na kulia kwa uchungu sana, na kusema, "Bwana, ninahitaji miaka kumi na mitano zaidi. Ninakusihi, Bwana, unisikie." Sasa, mfalme huyo alikuwa ndiye mtu mkuu kuliko wote ulimwenguni, katika siasa; lakini, nabii ndiye aliyekuwa mkuu kuliko watu wote, machoni pa Mungu. Huyo alikuwa mfalme wa Mungu; lakini alikuwa nabii wa Mungu. Kwa hiyo, Mungu alimfunulia nabii kuchukua baadhi . . . .kuchemsha baadhi . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] Mnajua, mnalipata?

331 Sasa, ili kwamba mpate kufahamu sasa, kwa sababu nimehubiri Maandiko hapa, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa katika kuja kwake Mwana wa adamu." Katika siku za kufunuliwa kwa kanisa? La! "Katika siku za kufunuliwa kwa Mwana wa adamu." *Kufunuliwa* ni nini? Kumtambulisha! Hiyo ni kweli? Kufunua! Siku atakapofunuliwa Mwana wa adamu, itakuwa ni siku kama ya Sodoma na Gomora. Hiyo ni kweli?

332 Sasa, angalia yaliyotukia. Walikuwa na wajumbe wawili wakuu, kule Sodoma na Gomora, kwa sababu kulikuwa na kundi la Wakristo vuguvugu kule. Hiyo ni kweli? Nao walikuwa na wajumbe wawili wakuu (sasa sikilizeni kwa makini) kule chini Sodoma na Gomora, wakihubiri. Lakini mmoja wao aliyesimama nje hapa pamoja na kundi la Ibrahimu. Hiyo ni kweli?

333 Sasa angalia! Kamwe hatujapata kuwa na mjumbe wa dunia nzima, katika historia nzima ya kanisa, ambaye jina lake liliishia kwa h-a-m, mpaka sasa: G-r-a-h-a-m, ambalo ni herufi sita, G-r-a-h-a-m. Lakini jina la Ibrahimu liliendelezwa: A-b-r-a-h-a-m, herufi saba. Unaona? Kwa hiyo kanisa la ulimwengu mzima, zikiwa herufi za mwanadamu, sita, madhehebu ya kujitengenezea, hata hivyo yamekwishapokea mjumbe wao. Wamekuwa na Sankey, Moody, Finney, Knox, Calvin, kadhalika, lakini kamwe si "h-a-m." Hiyo ni kweli? Lakini wamempata, naye ni mjumbe, aliyetumwa kutoka kwa Mungu, naye anazipondaponda kuta hizo kwa nguvu awezavyo, "Tokeni humu! Tubuni la sivyo mtaangamia!"

334 Lakini kumbukeni, Wateule, waliokusudiwa na kuchaguliwa kwa agano tangu zamani, Ibrahimu na kundi lake, walipata Mjumbe, pia. A-ha. Angalia yale aliyofanya. Yeye aliwapa ishara

ya kwamba wakati ulikuwa umekaribia kwa moto kushuka. Sasa, moto ndio tunaotarajia sasa, moto wa atomu, hasira ya Mungu.

335 Sasa, Mjumbe huyo alifanya jambo fulani. Alinena kuhusu mwanamke aliyekuwa amempa kisogo, na kumwambia—na kumwambia alikuwa anatilia shaka yale aliyokuwa anasema, akamwambia hali zake na jambo litakalotukia. Hiyo ni kweli? Je! Yeye alisema ya kwamba Mwana wa adamu atajifunua jinsi hiyo hiyo katika siku hiyo? Vema, mnaamini ya kwamba hiyo ni Kweli?

Vema, hapa panasimama mwanamke, . . .

336 Na katika muungano usioonekana wa Kanisa, Bibi-arusi wa Kristo, Mjumbe huyo yuko hapa sasa, ambaye ni Yesu Kristo, yeye yule jana, leo, na hata milele.

337 Sasa, Yeye hunena tu kupitia kwa manabii Wake. Biblia ilisema hivyo! "Yeye hafanyi lolote ila kwanza kuwafunulia manabii Wake," Amosi 3:7. Amefanya hivyo daima. Yeye kamwe habadilishi mpangilio Wake. Unaona? Naye nabii anaweza tu kunena, kama ni wa kweli, yale anayoambiwa na Mungu. Hiyo ni kweli? Hiyo ni kweli.

338 Sasa, je! mnaamini Yeye angeweza kuniambia mwanamke huyu ana shida gani kabla hata sijamwangalia? Mnaamini? Mbona, yeye ana ugonjwa na kansa. Hiyo ni kweli. Iko kwenye titi lake. Anawazia juu ya kijana, moyoni mwake, anaumwa na maradhi fulani ya ubongo, wasiwasi wa neva, na magonjwa yanayotokana na hali hiyo. Hiyo ni kweli. Unaamini jambo hilo? Na hiyo ni kweli, sivyo? Unaamini sasa ya kwamba imani yako iliyokuwa ikisema hivyo, imetia nanga, ya kwamba umeipata, utapokea jambo hilo? Basi nenda zako, na Bwana Yesu atakupa afya. Unaona? Naam. Unaona? Unaamini? Kwa moyo wako wote?

339 Sasa, mnaamini, bila kumwangalia mwanamke huyu, Bwana Yesu anaweza kuniambia shida yake ni nini? Ni wangapi wanaoamini jambo hilo? Sasa, mnajua . . . nami kamwe hata . . . mimi . . . jambo pekee, niliona tu sketi. Sijui, singeweza kusema kama ilikuwa ni mwanamume ama mwanamke; lakini anasimama tu pale. Ninataka aamini. Je! unaamini, mama? Hapa, mgonjwa huyu, unaamini? Inua mkono wako kama unaamini. Kama unaamini kwa moyo wako wote, unaweza kumpata mtoto huyo unayemwomba kwa Mungu. Unaona? Unaona? Unaamini? Unamwamini Mungu? Sasa, hilo haliponyi, hilo lilifichua tu. Hizo ndizo kazi zinazotambulisha imani ya Uwepo wa Mungu, Neno Lake likidhihirishwa.

340 Mwanamke huyu anataka kitu kikubwa sana, pia. Kitu hicho si mtoto mchanga, lakini anataka Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nitakwambia la kufanya. Kama ukiacha hizo sigara, Mungu

atakupa Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Nenda zako, amini jambo Hilo, unaona. Unaamini? Unamwamini Mungu?

341 Mwanamume huyu anayesimama hapa, ni mwanamume ambaye sijawahi kumwona maishani mwangu. Simjui, lakini ana shida fulani ndani ya kifua chake. Aliwahi kuanguka ambako kulisababisha hayo maumivu, si muda mrefu uliopita. Hatoki hapa, anatoka Arkansas. Yeye ni mhubiri. Nenda zako nyumbani, ukahubiri Injili. Unaona? Unaona? Unaona? Sijapata kuuona uso wa mtu huyu.

342 Kuna mwanamke anayesimama hapa, simjui mwanamke mwenyewe, sijapata kumwona maishani mwangu. Mungu anamjua.

343 Kama anaweza kufunua shida yake ni nini, ama kitu fulani juu yake, mngeamini? Ninyi nyote? Hii ni kazi tu inayotambulisha imani kwamba sina budi kuhubiri yale niliyowaambia, usiku wa leo. Hilo ndilo Mungu alilofunua, na hizi ndizo kazi zinazothibitisha jambo Hilo. Basi, huna budi kuwa na imani kusudi upate afya.

344 Mwanamke huyu hapa, si—sidhani ninamjua. Naam, mimi simjui bali ninajua mtu fulani ambaye yeye anamjua, maana ninamwona amesimama hapa mbele yangu. Anaumwa na kichwa. Sivyo, bibi? Unaamini ya kwamba Mungu atakuponya? Dada ya Pearry Green. Hiyo ni kweli. Sijapata kumwona maishani mwangu. Hiyo ni kweli. Nilimwona Pearry Green amesimama hapa, akiniangalia, akifanya namna *hiyo*. Ndio kwanza aje, unaona. Sawa. Sijui Pearry Green yuko wapi. Unaamini? Unaamini kiasi gani? Kama unaweza kuamini, yote yanawezekana. Kama hamwezi kuamini, hakuna kinachoweza kutendeka.

345 Huyo maskini bibi mwenye nywele zenye mvi, anayeketi pale akiniangalia, papa hapa, je! unamwamini Mungu? Je! unaamini ya kwamba Mungu anaweza kunifunulia kile unachowazia hapo? Una kivimbe kwenye titi. Unaamini Mungu anaweza kukiondoa kutoka kwako? Naam. Uwe na imani na uamini. Sasa, yeye aligusa kitu gani?

346 Mwanamke yule aliyegusa upindo wa vazi Lake, Biblia ilisema . . . Ninyi ambao mnataka kufungua Biblia, Yeye alisema, "Yeye ni kuhani Mkuu anayeweza kuchukuana nasi katika mambo yetu ya udhaifu." Hiyo si ni kweli? Yeye ndiye Huyo Kuhani Mkuu naye anasimama papa hapa, sasa watu wanamgusa.

347 Kuna maskini mwanamke mdogo, mwembamba, aliyeinua mkono wake, anayeketi papa hapa. Sijawahi kumwona maishani mwangu, lakini amekwisha kugusa kitu fulani. Hivi ndivyo ilivyokuwa. Anamwomba Mungu. Ana shida ndani ya kifua chake, na pia anaumwa na tumbo. Mungu alikuponya, kama

utaamini. Huna budi kuamini. “Mambo yote yanawezekana kwa hao waaminio.”

348 Kuna mwanamume anayeketi huko nyuma kabisa, akiangalia huku (karibu safu ya pili, kuja hivi), ana ugonjwa wa pumu. Unaamini Mungu atakuponya, bwana? Kama unaamini, Mungu atakuponya. Unaweza kupata ulichoomba, kama ukiamini.

349 Kuna mwanamke anayeketi papa hapa, akiniangalia mimi, upande wa pili hapa, ana mvi. Kama ukiamini kwa moyo wako wote . . . Unaamini? Vyema, huo ugonjwa wa kibofu nyongo utakuacha basi, kama ukiamini.

350 Unafikiri nini juu ya Hilo, unayelala hapa kwenye kitanda kidogo? Unaamini ya kwamba Mungu anaweza kukuponya? Kama Mungu ataniambia shida yako, je! utamwamini Yeye? Kama utaamini, kansa hiyo itakuacha nawe utapona. Mbona usiinuke, na kuchukua kitanda chako, na uende nyumbani? Unaamini? Ninyi nyote mtaamini? Vema, sasa, vipi sasa hivi? Je! Mungu ameidondosha hiyo imani moyoni mwako? Kila mtu hapa ndani, inua mkono wako. Kama Mungu aliidondosha hiyo imani moyoni mwako, na tuwekeane mikono sisi kwa sisi, moja kwa moja hapa kwenye mstari. Wekeaneni mikono . . . Sasa hivi, upesi, wakati Roho Mtakatifu anatenda kazi, wekeaneni mikono ninyi kwa ninyi. Mtu huyo ameamka, anakimbia mstarini, akiwaombea wengine.

351 Hebu na tusimame kwa miguu yetu na tumpe Mungu sifa, kila mtu. Hakuna haja ya kuendelea mbele zaidi. Mtambulishe Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele. Wewe, kwamba mateso yako ni nini, yoyote yale, kama unamwamini Yeye, simama kwa miguu yako, sasa hivi, na uamini.

352 Mwenyezi Mungu, Mungu wa Ibrahimu, Mungu wa Isaka, Mungu wa Yakobo, tuma nguvu Zako na uponye kundi hili la watu sasa hivi, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

Mungu atukuzwe! Mungu awabariki!

Kazi Ni Imani Katika Matendo SWA65-1126
(Works Is Faith Expressed)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa Ijumaa jioni, tarehe 26 November, 1965, katika Maskani ya Uzima huko Shreveport, Louisiana, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings.

SWAHILI

©2010 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org